

MALKIA WA SHEBA



Hebu na tuendeleo kusimama kwa muda kidogo tunapoomba, na tuinamishe vichwa vyetu.

² Baba yetu wa Mbinguni mwenye Rehema, tunakushukuru Wewe kwa ajili ya majaliwa haya makuu ya kukikaribia kiti Chako cha rehema tena usiku wa leo, katika Jina litoshelezalo kwa yote la Yesu, Mwanao. Tunakushukuru Wewe kwa sababu tuna hakikisho kamili ya kwamba kama tukiomba lolote katika Jina Lake, tutajaliwa. Kwa hiyo, kuna wengi hapa usiku wa leo ambao ni wahitaji, ni wagonjwa katika mwili, baadhi yao ni wagonjwa katika nafsi, tunaomba, Baba, ya kwamba Wewe utawapa kila kitu wanachohitaji, wokovu kwa ajili ya nafsi zao kuliko vitu vyote, kisha uponyaji kwa wagonjwa, furaha kwa wale wanaohuzunika, tumaini kwa wale wasio na matumaini. Tujalie, Bwana.

³ Na wakati ibada itakapokwisha usiku wa leo, nasi tuende kwenye makazi yetu mbalimbali, mahali tunapoishi, jalia tuseme kama wale waliotoka Emau siku ile, “Je, mioyo yetu haikuwaka ndani yetu, hapo alipokuwa akisema nasi njiani?” Kwa kuwa tunaomba, katika Jina la Yesu. Amina.

⁴ Mnaweza kuketi. Ni majaliwa makubwa sana kurudi hapa tena, usiku wa leo, katika Ukumbi huu wa Manispaa ya Long Beach. Imekuwa miaka kadhaa tangu nilipokuwa hapa, yapata mwaka wa '46 ama '47, mahali kama hapo. Ninaamini nilifuata ibada ya mtumishi mashuhuri wa Bwana, Dk. Charles Fuller, alikuwa na yale *Majira Ya Uamsho Wa Mtindo Wa Kale*, yalikuwa yakianza, nayo yalibuniwa hapa, mtumishi mashuhuri wa Bwana. Nasikia sasa ya kwamba hafanyii ibada zake hapa tena. Daima nilitaka kukutana na Ndugu Fuller, kamwe sikupata majaliwa hayo makuu.

⁵ Ninakumbuka nikija Afrika Kusini yapata miaka saba ama minane iliyopita, kusanyiko la yapata watu elfu mia mbili hamsini. Ninyi, baadhi yenu watu wa Long Beach, kamwe msingeweza kukisia walinisalimia na nini nilipokuja jukwaani, wakiimba katika yapata lugha kumi na tano mbalimbali, zote zikichanganyika pamoja: *Mwanga wa Jua la Mbinguni*. Walikuwa wakiimba *Mwanga wa Jua la Mbinguni*, ambao ninaamini ulikuwa ndio wimbo rasmi wa Dk. Fuller hapa.

⁶ Nami daima niliwazia kama ngingekutana naye, ningetaka kumwambia kwamba, kwamba jumbe zake zilikuwa zimefika huko chini, huko chini kabisa Afrika Kusini. Nao hao watu wa thamani walimpenda, na walijua mimi nikiwa Mmarekani, waliimba *Mwanga wa Jua la Mbinguni*, ama *Mwangaza wa Jua*, vyovyote uendavyo. Nao walikuwa wakiuimba katika

lugha kumi na tano mbalimbali kwa jumla. Loo, kamwe huninii...Lakini zote zikichanganyikana kikamilifu kabisa. Roho Mtakatifu, wakati watu wanapokusanyika pamoja nao upendo wa Mungu unapoanza kutenda kazi juu yao, hakuna mgongano, wote ni Mwili mmoja mkubwa, ukisonga pamoja.

⁷ Dk. F. F. Bosworth, ambaye ni mmoja wa mameneja, alisimama tu, akaongoza taarabu, alikuwa akichukua bendi ya Dowie, bendi ya watu sabini na watano huko Madison Square Garden katika siku za Dk. Alexander Dowie, naye alisema alikuwa ameifundisha hiyo kwaya, nawe ungepata mtu fulani anaimba oktava chache juu, ama chochote mnachoiita, juu, na wengine chini sana, lakini kasema katika hao makafiri watupu, wenyeji wavaao blanketi, wasiojua mkono wa kulia na wa kushoto ni upi, huku wanapigana wao kwa wao, iliwabidi kuwatenganisha katika makabila, hata hivyo hawakuwa na oktava moja nje hata kidogo, kila mtu akichanganyikana moja kwa moja pamoja, *Mwangaza wa Jua la Mbinguni*.

⁸ Kama mtu yeyote anamjua Ndugu Fuller, mwambie hilo kwa niaba yangu. Sidhani nitaninii...huenda kamwe nisimwone, yeye ni mtu mwenye shughuli nyingi, nami sipendi kuchukua huo wakati, lakini bila shaka lingemsisimua.

⁹ Injili, na hata hivyo katika urahisi wake ndiyo kadi kuu sana ya kuwavuta watu ambayo ulimwengu umewahi kujua. Yesu alisema, wakati alipokuwa hapa duniani, "Nikiinuliwa juu, nitawavuta watu wote Kwangu." Weusi, weupe, manjano, hudhurungi, chochote ilicho rangi yao ama jamii, Injili ingali inashikilia kiini cha mvuto kwa kila mwanamume na kila mwanamke.

¹⁰ Nami ninaamini ya kwamba makanisa yetu yanapaswa kuwa yameendelea tu mbele kidogo katika Injili kuliko tulivyo. Nafikiri kwamba tunachangia hilo, nafikiri, na kama nimekosea, naomba Bwana anisamehe, nafikiri tunajaribu kuangalia nyuma sana kuona kile mtu mwingine amefanya, ama kusema, badala ya kumtazamia Kristo, Yeye ndiye Kiongozi wetu.

¹¹ Miaka mia chache iliyopita, huenda nikakosea katika nukuu hii, lakini ningesema miaka mia tatu iliyopita, ninaamini ilikuwa ni mwanasayansi huko Ufaransa aliyejaribu kuchukua mpira na kuuzungusha duniani, ama *kitu kingine*, huenda ilikuwa ni miaka mia moja na hamsini iliyopita, aliuzungusha duniani na, kwa mwendo fulani, na kudai kama gari lolote duniani lingewahi kwenda mwendo wa kasi sana wa maili thelathini kwa saa kwamba nguvu za uvutano zingepoteza mshiko wake, lingendoka moja kwa moja duniani. Sasa, hilo lilithibitishwa kisayansi katika siku hiyo. Mnafikiri sayansi yoyote ingeangalia nyuma, na kusema...kwa hilo? La hashu. Ninaona mahali ambapo wana ndege sasa, ninasahau, yapata

maili elfu tano kwa saa kwa zingine. Nao hata hawakomei hapo, wanazidi kuendelea mbele zaidi, na zaidi.

¹² Lakini sisi Wakristo, na sisi makasisi, na wahudumu, tunajaribu kuangalia nyuma katika shule yetu na kuona kile Bw. Moody alichosema juu yake, Bw., yale Bw. Sankey aliyosema, ama—ama Finney, ama Knox, ama Calvin, ama yeyote wa hao. Sasa, walikuwa watu mashuhuri katika siku zao, lakini, mnaona, daima tunaangalia nyuma, hebu na tuangalie mbele. Mnaona? Tuna rasilimali zisizotumiwa.

¹³ Na sasa, sayansi inaweza tu kupanda *juu kiasi fulani*, ndipo inawabidi kuondoka, kurudi nyuma, mti wa maarifa huzaa tu *kiasi fulani*, ule uliowekwa mbele zetu katika bustani ya Edeni. Naye mwanadamu ana kawaida ya kuishi kwa mti huo wa maarifa, lakini kamwe haikuwa ni mpango wa Mungu kwetu kuishi kwa mti huo wa maarifa. Mara ya kwanza mwanadamu alipouma kutoka kwenye huo mti wa maarifa, alitenganisha ushirika wake na Mungu. Kila wakati anapouma mti huo, anajiangamiza mwenyewe, daima. Aliuma baruti, angalia kile hiyo inafanya, anamwua mwenzake; akauma motokaa, hiyo inaua zaidi ya baruti; sasa ana bomu la atomiki, na la haidrojeni angali anakula kutoka kwenye mti huo wa maarifa ambao, hatimaye, utamrudisha kwenye kikomo chake.

¹⁴ Lakini ule Mti wa Uzima aliouacha, makusudi, apate kula kutoka kwenye mti wa maarifa, basi hapo ndipo anapoondoka peke yake. Ninaamini ya kwamba sayansi sasa . . .

¹⁵ Nilichunguzwa kwa moja ya vipimo hivyo vya mita mikononi mwako kuhusu Nuru hii, Malaika wa Bwana. Ndipo ikapigwa picha ya kisayansi, mnayo papa hapa sasa, imepigwa kote ulimwenguni mahali mbalimbali, picha ya Nguzo ile ile ya Moto iliyowafuata wana wa Israeli, iliyothibitishwa kisayansi. George J. Lacy, mkuu wa FBI wa alama za vidole pamoja na hati, mnaona, aliichunguza aone kama ilikuwa sahihi, akasema, “Si saikolojia,” akasema, “jicho la kimitambo la hii kamera halitapiga picha saikolojia.”

¹⁶ Sasa, badala ya kusonga mbele na kuona yale Mungu aliyoahidi, tunaangalia nyuma na kuona yale ndugu fulani nyuma yetu alisema, hebu tusiangalie nyuma, tuangalie mbele, tuendeleo kusonga mbele, mbele. Tuna rasilimali zisizotumiwa, Yesu alisema katika Marko Mtakatifu 11:23, “Lolote—lo- . . . Ukiuambia mlima huu, ‘Ng’oka,’ wala usione shaka moyoni mwako, bali uamini ya kwamba yale uliyosema yatatimia, yatakuwa yako.” Hakuna—hakuna masharti, si—si . . . ni kwamba tu hayana kikomo. “Yoyote mtakayo, mkisali, aminini ya kwamba mnayapokea, yatakuwa yenu,” chochote kile, uponyaji wa Kiungu, furaha, amani, chochote kile.

¹⁷ Sasa, mnasema, “Ndugu Branham, vipi kama tungeomba kitu ambacho . . . kwamba uhai wa mtu fulani uchukuliwe, ama

kitu kiovu.” Vema, kweli usingeweza kuwa na imani ya Kikristo kwa kitu kama hicho, inahitaji roho ya Kikristo kuomba mambo ya Kikristo, kupokea vitu kutoka kwa Kristo. Inakubidi kuwa na...

¹⁸ Daima kumbukeni, enyi kanisa, Maneno ya Mungu ni ya kweli. Ninaamini mtazamo mzuri wa kiakili wa ahadi yoyote ya Kiungu ya Mungu utaitimiza, kama unaweza kuiangalia kwa njia ifaayo.

¹⁹ Lakini kumbukeni, hiki kimekuwa kigezo cha—changu maishani, nimejaribu kufanya hivi: Jambo la kwanza, ninataka kujua kama ni mapenzi ya Mungu au la, ndipo—ndipo ninajua ni mapenzi ya Mungu; jambo lingine, ni kusudi langu kwake, na nia yangu katika kulifanya; ndipo kama ni mapenzi ya Mungu, na kusudi langu ni zuri, na nia yangu ni nzuri, nina imani ya kwamba itatendeka. Kwa sababu, kwanza, ni mapenzi ya Mungu, nami nina ninii... na kusudi langu ni kumtukuza Yeye, na kusudi langu ni kumpa Yeye utukufu wote. Mnaona? Kwa hiyo hakuna nia ya ubinafsi juu yake, kama una nia ya kichoyo haitafanikiwa. Kama lengo lako ni kujipatia pesa, ama kitu fulani, mbona, kamwe hutafanikiwa. Na kisha kujaribu kufanya jambo fulani nje ya mapenzi ya Bwana, basi kwanza kabisa halitafanikiwa.

²⁰ Kwa hiyo kuna imani ya kweli, lakini lazima uingie kwenye mkondo halisi wa Mungu upate kuwa na imani hiyo halisi. Kuna imani ya kibinadamu, halafu kuna imani ya Mungu, nawe huna budi kuwa na imani ya kiungu kuamini, sio... Basi ili kuwa na imani ya kiungu, inakubidi kuwa na nia ya Kristo ndani yako, basi hivyo ndivyo Mungu anavyokuwekea maono, mafunuo, na mambo haya yote, huja wakati nia ya Kristo ikiwa ndani yako. Mnalipata? “Nia iliyokuwamo ndani ya Kristo na iwe ndani yenu.”

²¹ Vema, inanisisimua, usiku wa leo tena, kusema kurudi hapa Long Beach baada ya miaka mingi. Ninakumbuka wakati nilipoingia hapa kwa mara ya kwanza, kulikuwa na shaka chungu nzima kuhusu huduma, ningekuwa karibu ndiye pekee hudumani wakati huo aliye na miamsho ya uponyaji. Ninakumbuka jinsi ilivyokosolewa sana. Nami ninakumbuka ule usiku nilipoondoka hapa, nami nikausikiliza ujumbe wa kusiona wa Dk. Fuller, niliketi moja kwa moja hapa nje alasiri hiyo na kusikia ujumbe wake mkuu, wa kusiona, wa nguvu wa mafundisho.

²² Nikaona kusanyiko lake likiondoka, watu wazuri, wenye akili, wenye sura nzuri, watu safi, nikawaona wote wakiondoka kwenye jengo, hilo lilikuwa kusanyiko lake, sasa hili hapa langu linaingia, wendawazimu, kwenye viti vya magurudumu, hmm! Nikawazia, “Hilo ni jambo dogo sana tofauti kabisa kutegemeza hiyo, imani yako,” mnaona, hatuna budi kujua. Lakini ilikuwa

changamoto kwa Neno la Mungu ambalo Mungu ameahidi kwamba ilikuwa ni kweli, Naye angesimama nyuma yake. Kote ulimwenguni nimekuwa na Ujumbe huu, hakuna hata wakati mmoja ambapo Mungu amewahi kushindwa.

²³ Na baada ya yapata miaka kumi na minne tangu niwe humu ndani, ninasimama, usiku wa leo, nikiwa na ujumbe ule ule kwa Long Beach, niliokuwa nao nilipokuja hapa: “Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele.” Yeye ni—Yeye hajapungua hata kidogo, hajawahi kunipungukia. Nimesimama mbele ya wachawi na pepo, na, kunywa damu katika fuvu la kichwa cha mwanadamu na kumwita ibilisi, na kukupa changamoto moja kwa moja, wala sijawahi kuona wakati mmoja ambapo changamoto iliwahi kutolewa pasipo Mungu kujitokeza jukwaani na kufanya jambo kuu. Na—naisai imani yako, usiku wa leo, kumwamini Bwana Yesu.

²⁴ Tumekuwa na juma kuu, ama, majuma mawili, pamoja na Ndugu Buntain wa Kanisa la Assembly of God hapa mjini. Nimejifunza kumpenda Ndugu Buntain kama vile ndugu anavyoweza tu kumpenda mwingine. Sikumjua kabisa nilipoingia hapa, nilikuwa nimesikia juu ya baba yake hodari huko Canada, ambaye ni mtu mashuhuri, mtumishi wa Kristo. Ndipo nikakutana na ndugu yake, nilikuwa na majaliwa hayo; nilikutana na ndugu wengine hapa na kufanya ushirika pamoja nao. Uimbaji mzuri, wahudumu wazuri, maskini yule mama ambaye ndiyo kwanza aimbe, Bibi Piper, ninaamini ndilo jina lake, sauti nzuri kweli, unapaswa kuwa wakati wote unamwendea Kristo, kila mahali, mambo haya yote yanapaswa kuwa yakitenda kazi kwa kuwa kidogo kumechelewa kuliko mnavyodhania. Ninaamini tuko karibu na . . .

²⁵ Je, ninasimama karibu sana na maikrofoni? Mnaweza kunisikia vizuri zaidi nikirudi nyuma namna hii? Hiyo ni bora zaidi? Vema. Sininii, ninawatakeni msikie yale ninayonena, bali sitaki sauti yangu irudishe mwangwi. Sasa, mazingira sikizi hapa kwa kawaida ni mazuri sana, yalikuwa hivyo mara ya mwisho tulipokuwa hapa.

²⁶ Ningetaka kurudi wakati mwingine, kama ingempendeza Mungu, mapenzi ya Mungu, na kuwapendeza watu, na labda tupate mahali kama hapa, badala ya kuwa na kanisa moja tu likidhamini, wote waudhamini, na ndipo tungeweza kuja hapa kwa ajili ya mkutano mkubwa mno. Nitaombea jambo hilo kama mtaomba vivyo hivyo. Halafu basi—basi labda tungeuweka mbali vya kutosha kabla ya wakati mpaka, tungeweza kupata wadhamini wa thamani, ama wowote wale, wasimamizi wa jumba hili la mikutano sasa, kwa kuwa wanajenga moja kubwa zaidi hapa nje, ambapo tungeweza kulitumia wakati mwingine kwa mkutano wa siku kumi, ama chochote kile. Ninaamini ya kwamba ingekuwa ni vema sana kuja; chochote ambacho kingekuwa cha kupendeza, ama kumfanyia Mungu jambo fulani.

²⁷ Na sasa, nilipotaja dakika chache zilizopita Assemblies of God, sasa hilo ni kanisa moja tu la kimadhehebu. Hatuninii... Kwangu mimi mwenyewe, kama kila mtu ajuavyo, ya kwamba nilitawazwa nikiwa na umri wa kama miaka ishirini na mmoja, na hiyo imekuwa yapata miaka thelathini na mmoja iliyopita katika kanisa la Kimishenari la Kibaptisti; ambao sina chochote kiovu ambacho ningeweza kusema juu ya kanisa la Kibaptisti la Kimishenari, ama dhehebu lingine lolote.

²⁸ Nimechukua msimamo huu, kwamba kama kanisa Katoliki, Mkatoliki, Mkatoliki wa Kirumi, ama mwothodoksi, ama chochote awezacho kuwa, kama anatazamia kanisa Katoliki kwa ajili ya wokovu, mtu huyo amepotea; kama Mbaptisti anatazamia kanisa la Kibaptisti kwa ajili ya wokovu, amepotea; kama Mpentekoste analitazamia kanisa la Kipentekoste kwa ajili ya wokovu, amepotea, lakini kama Mkatoliki, Mpentekoste, ama Mbaptisti, Mpresbiteri, ama yeyote yule, kama anamtumainia Yesu Kristo kwa uchaji, ameokoka, kwa sababu ni kwa imani unaokolewa, na hiyo ni kwa neema. Unaona?

²⁹ Wakatoliki wanaweza kuokoka, Wabaptisti wanaweza kuokoka, Wapentekoste wanaokoka, kwa sababu sisi sote tunakubali yale Kristo aliyotufanyia. Hiyo ni kweli. Ni imani yetu wenyewe katika kazi iliyomalizika ambayo Kristo alitufanyia, kwa hiyo kamwe sijaweka mpaka wa kimadhehebu wala kuwa na kizuizi, nimejaribu kunyosha mkono, kumchukua kila mmoja mikononi mwangu na kuwaelekeza msalabani, sasa, na hiyo ni:

Mpendwa Mwana-Kondoo anayekufa, Damu
Yako ya thamani
Kamwe haitapoteza nguvu zake,
Mpaka Kanisa lote la Mungu lililokombolewa
Litakapookolewa lisitende dhambi tena.

Tangu kwa imani nilipokiona kile kijito,
Kilichosababishwa na majeraha yako,
Upendo wa ukombozi umekuwa ndio wimbo
wangu,
Na utakuwa hivyo mpaka nitakapokufa.

³⁰ Huo ndio—huo ndio wito wangu, huenda nikasema, halafu tena: Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele.

³¹ Asanteni nyote kwa wema wenu wote na rehema, na ushirikiano wenu mkarimu ambao mmenipa mimi, na—na mambo mazuri ambayo mmefanya, na barua zenu, nasi tunazijibu upesi tu tuwezavyo. Na vile vitambaa vidogo vya kuombea ambavyo nimeviombea, vingi vya hivyo sijavitoa bado. Na kama unataka kimoja, ni bure kabisa, niandikie tu huko Jeffersonville, Indiana, nami nitakutumia kimoja. Kama tu wewe... Sanduku la Posta 325. Lakini kama huwezi

kulikumbuka hilo, ni Jeffersonville tu, Indiana, ni mji mdogo, wenye watu kama thelathini na tano elfu, na barua zetu ni nyingi mno.

³² Sasa, sijaribu kuchukua anwani yako, kwa kuwa sina miradi yoyote, sina chochote, sina mipango. Tuna vitabu, lakini hivyo vitabu, tunavinunua kutoka kwa mtu mwingine kuvileta mkutanoni. Sina redio, sina televisheni, sina chochote kile. Siwajibiki kwa chochote ama mtu yeyote ila Mungu pekee. Mnaona? Ninaweza kwenda kanisani, dogo au kubwa, si lazima niwe na kiasi fulani cha pesa, hakuna kitu kilichotengwa.

³³ Nina umri wa miaka hamsini na mmoja, nimekuwa nikihubiri miaka thelathini na mmoja, wala kamwe sikuchukua sadaka maishani mwangu. Hiyo ni kweli. Mi—mimi. . . Hakuna pesa zilizohusishwa kwake hata kidogo. Watu hunipa vitu vidogo ili niweze kuishi kwavyo, na kusaidia huduma, ambayo inathaminiwa, hizo zinaingia kwenye wakfu mmoja kanisani mwangu. Mimi mwenyewe, ninapata dola mia moja kwa juma kwa ajili ya riziki yangu, na nje ya hizo, vema, hizo tu ndizo nilizo nazo, na hizo tu ndizo ninazohitaji.

³⁴ Wala si—siamini ya kwamba Injili ya Kristo ilipata kufanywa ya kufanyia biashara, ninaamini ya kwamba haipaswi kufanywa. Nami siamini ya kwamba—ya kwamba watumishi wa Kristo wanapaswa kujaribu kuwa watu wa maonyesho, ninaamini wanapaswa kuwa wanyenyekevu, wachukue mahali pa Kristo, Ambaye sisi, Uhai Wake ndani yetu, unamwakilisha Yeye kwa umma.

³⁵ Sasa, tunaona ya kwamba Yeye alisema, “Mbweha wana mashimo na matundu, na ndege wana viota; bali Mwana wa Mungu hana mahali pa kulaza kichwa Chake.” Haikumbidi kuwa hivyo. Nafikiri Neno lililo tamu sana katika Biblia, moja la hayo, “Baba, najitakasa Mwenyewe kwa ajili yao.” Alikuwa na haki ya kuwa na mke, alikuwa na haki ya kuwa na nyumba, alikuwa na haki kwa—kwa anasa za maisha, kama tulizo nazo, angalau anasa za maisha, bali alikuwa akijitakasa Mwenyewe kwa sababu alikuwa akiwafundisha watu kumi na wawili ambao wangeuchochea ulimwengu kwa Injili. Na kama angeweza kufanya hivyo, ni zaidi sana vipi sisi tunavyopaswa kujitakasa? Bila shaka.

Sasa, hebu, neno moja tu zaidi Kwake. Kabla hatujalikaribia Neno la Mwandishi, hebu na tumkaribie Yeye mara nyingine tena katika maombi.

³⁶ Bwana, ni Neno Lako, tunaomba ya kwamba utalifanya halisi kwetu usiku wa leo. Sasa, tunajua ya kwamba imeandikwa, ya kwamba, “Mtu hataishi kwa mkate pekee, bali kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu.” Na tunapolisoma Neno Lako, tunajua halitashindwa. Maneno yetu yatashindwa kwa sababu sisi ni wanadamu na tuna

kikomo, bali Wewe ni Mungu wa Milele, asiye na kikomo, na asiyepatikana na mauti. Na ninapolikaribia Neno Lako, ninalikaribia chini ya imani ya namna hiyo, kwamba Maneno Yako hayawezi kushindwa. Na kama nikisoma Neno hili, basi kama watu waliokusanyika hapa usiku wa leo wakienda nyumbani, wanaweza kusema angalau walisikia kitu cha Milele, kwa sababu kilikuwa ni Neno Lako.

³⁷ Basi, Baba, kama Injili ilikuja si kwa kusikia tu Neno, imani ilikuja kwa njia hiyo, bali Injili ilikuwa idhihirishe, ama kuonyesha, nguvu za Roho Mtakatifu zilizo katika Neno. Kwa kuwa, “Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu.” Ndipo tunafundishwa katika Kitabu cha Waebrania ya kwamba Neno la Mungu ni kali kuliko upanga ukatao kuwili, likikata, hata kwenye mafuta ya mfupa, nalo Neno la Mungu ni Mtambuzi wa mawazo ya moyo.

³⁸ Makusudio ya mioyo yetu na nia zetu, Neno la Mungu linaweza kuyafunua, kwa sababu Kristo aliye hai, Yeye aliye Neno lililo hai, anaingia ndani ya nafsi yetu iliyo hai, hufunua siri za moyo, kwa kuwa Yeye ni Neno. Jalia Neno linene, Baba, na mawazo ya moyo wetu yapate kibali mbele Zako, Ee Bwana. Kwa kuwa tunaomba, katika Jina la Yesu. Amina.

³⁹ Katika Kitabu cha Injili ya Mathayo Mtakatifu, mlango wa 12, kifungu cha 42, tutasoma hili kwa sehemu, uh, kwa ajili ya somo:

Naye malkia wa kusini atasimama siku ya hukumu pamoja na watu wa kizazi hiki, naye atawahukumu kuwa wamekosa: kwa sababu yeye alikuja kutoka pande za mwisho za dunia ili asikie hekima ya Sulemani; na, tazama, hapa yupo aliye mkuu kuliko Sulemani.

⁴⁰ Yesu, katika masomo yaliyotangulia hapa, natamani wakati ungeenda nyumbani, usome sura hii tukufu, naye Yesu alikuwa akiwakemea na kuwakaripia, kwa sababu hawakuwa wamemwamini. Yeye alikuja, Yeye alisema, katika Jina la Baba Yake, nao hawakumpokea, akasema, “Mwingine atakuja kwa jina lake mwenyewe, na ndipo mtampokea.” Na hiyo ni kweli.

⁴¹ Tunakuja na kufanya makanisa yetu na kuwa na madhehebu yetu, nao wananinii. . . mko tayari kusema, “Naam, mi—mi—mi—mimi ni mfuasi wa Baptisti, Presbiteri.” Unapokea hilo kwa urahisi hivyo, bali kumpokea Yesu, uh—uh, hawamtaki.

⁴² Sasa, Yeye alisema, “Naja.” Na wakati alipokuja, watu hawakumtambua, alikuja jinsi hasa Maandiko yalivyosema ya kwamba angekuja. Yeye alikuja na alikuwa Masihi wa Kiyahudi. Wala si Masihi wa Kiyahudi tu, Yeye alikuwa Uzao aliyeahidiwa wa Ibrahimu, ambapo tumepitia juma hili la masomo, na, huko kanisani. Naye alikuja kwa walio Wake, nao walio Wake hawakumpokea.

43 Naye alikuwa amejitoa Mwenyewe kwa walio Wake. Naye aliwajia Israeli, ambao walikuwa ka—kanisa la Mungu, na watu wa Mungu, na taifa la Mungu, “Naye alikuja kwa walio Wake wala walio Wake hawakumpokea, bali wote waliompokea, aliwapa uwezo wa kufanyika wana wa Mungu, ndio wale walioliamini Jina Lake.”

44 Sasa, tunaona ya kwamba kulikuwako na matabaka matatu ya watu. Tunatokana na wana watatu wa Nuhu: Hamu, Shemu, na Yafethi; na kulikuwako, hao walikuwa ni Myahudi, Mmataifa, na Msamaria.

45 Kama ukiangalia, Petro, kwa ufunuo, alipewa funguo za Ufalme, kwa sababu Mungu alijua ya kwamba alikuwa na ufunuo wa Maandiko, kwa kuwa aliwauliza wanafunzi Wake wote, “Watu huninena mimi Mwana wa Adamu kuwa ni nani?”

Ndipo mmoja akasema, “Wewe ni Eliya.”

Na huyo mwingine akasema, “Wewe ni yule nabii.”

Na mmoja akasema, “Musa.”

Akasema, “Lakini ninawauliza, ninyi mwasema Mimi kuwa ni nani?”

Ndipo Petro akasema, “Wewe ni Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai.”

46 Naye Yesu akasema, “Heri wewe, mwana wa Yona, mwili na damu havikukufunulia hili, bali Baba Yangu aliye Mbinguni.” Mnaona, ilikuwa ni ufunuo. “Na juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu, na malango ya kuzimu hayawezi kulishinda.” Mnaona? Ilikuwa ni ufunuo wa moja kwa moja uliokuwa umejulishwa mtume, ya kwamba Yeye alikuwa ni Mwana wa Mungu.

47 Sasa, kama Kanisa la Mungu lingalipo, basi wale walio ndani ya Kanisa wameingia mle kwa ufunuo wa kiroho, kwa sababu hivyo ndivyo tunavyoingia Kanisani. Lakini wengi wetu hujaribu kuingia kupitia theolojia ya mafundisho, na *hivi-hivi*, na vema, ambalo sisemi neno dhidi ya hilo, lakini ninajaribu kutofautisha kati ya kile kilicho kweli *hasa*, na kilicho kweli kwa *sehemu*. Ufunuo ambao Mungu anakufunulia ya kwamba Huyu ni Mwanawe aliyekufa badala yako, basi huo ndio ufunuo, kwamba Yeye ni Nani.

48 Sasa, Yesu alikuwa amekuja na alikuwa amewathibitishia watu kwa kila njia ambayo Maandiko yalikuwa yamesema, ya kwamba Yeye alikuwa ndiye Masihi aliyekuwako... waliyemtazamia kuja. Sasa, wengi wao walikuwa wamechukua dhana mbaya ya kuja Kwake, na hiyo ndiyo sababu Yeye alieleweka vibaya. Samahani kwa tamshi hilo, lakini hiyo ndiyo sababu usiku wa leo Yeye anaeleweka vibaya, wanapata wazo baya la kile Yeye alichu.

⁴⁹ Sasa, ninaamini nilipokuwa nimesimama pale, nilimsikia mwenzangu hapa, akisoma Maandiko ya msemo kwamba mada za huu uamsho daima ni, “Yesu Kristo yeye yule jana, leo, hata milele,” alinukuu Waebrania 13:8 kwamba “Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele.”

⁵⁰ Sasa, Yeye alipokuja wao, lile—lile kundi kubwa la Israeli bila shaka lilikuwa limefungua macho likimtazamia Masihi, bali walikuwa wakimtazamia jinsi walivyokuwa wamefundishwa kwamba angekuja. Vema sasa, mtu yeyote mzuri, mwenye mawazo ya kiroho, ama hata mtu mwenye mawazo ya kiakili, angejua ya kwamba Yeye hakuja kinyume na Maandiko, Yeye alikuja kinyume na *ufahamu* wao wa Maandiko, si kinyume na Maandiko, lakini walikuwa wamefundishwa na walimu wao kwa njia ambayo hao walimu walikuwa—walikuwa na dhana mbaya juu Yake.

⁵¹ Na hebu nisiumize hisia kwa kusema jambo hili, lakini labda huenda ikawa hivyo tena. Mnajua kama Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele, labda atakuja tofauti kidogo na vile tunavyomtarajia kuja. Hiyo ni njia tu ya—ya kimantiki, ya busara, ya kuliendea wazo kama hilo, ningeamini, katika siku hii.

⁵² Sasa, tutaona basi ya kwamba wakati alipokuja, Masihi alipaswa kuwa, kulingana na nabii Musa, ambaye kweli ndiye aliyetabiri kuja Kwake na kusema, “Bwana Mungu wenu atawaondokeshea Nabii kama nilivyo mimi.” Sasa, mwanatheolojia yeyote mzuri angalijua ya kwamba ilibidi Masihi huyo awe ni Nabii, ama ninii Zake—ama sifa Zake zilizomfuata zingekuwa za kinabii, kwa sababu kwamba Israeli daima waliamriwa kuwaamini manabii wao, daima wangewaamini.

⁵³ Lakini inatubidi kuzingatia hili, pia, ya kwamba si wote wanaoweza kumjia Kristo, kwa kuwa Yeye alisema, “Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu asipovutwa na Baba Yangu kwanza. Na wote alionipa Baba watakuja Kwangu.” Angalia mamilioni waliopokea . . . ambao hawakumpokea katika siku hiyo, na wale wachache waliompokea. Sasa, hebu na tuliweke hilo kwenye leo hii, na tuliangalie kwa makini jinsi linavyopaswa kuwa.

⁵⁴ Sasa, tunaona wakati akija kwamba alifanya ishara ya Masihi. Na mara nyingi juma hili tumejaribu kutoa hilo na kulionyesha tena, na tena, na mara nyingine tena, kote kutoka Mwanzo hadi Ufunuo tulilion. Je, hiyo ni kweli, enyi darasa, juma hili? Kwamba kile Masihi angekuwa . . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

⁵⁵ . . . tulitiwa mafuta . . . Nabii daima ana Neno la Bwana, nabii wa kweli. Mnaona? Nabii alisema ya kwamba “Wana macho, wala hawawezi kuona,” wasingeweza kuona miujiza, “wana masikio, wala hawawezi kusikia.” Mnaona? Isaya alisema

hivyo, kwa hiyo tunajua basi ya kwamba—ya kwamba iliwabidi kuwa hivyo. Si kwamba Mungu alikusudia iwe hivyo, bali kwa kujua Kwake tangu zamani Yeye alijua ingekuwa hivyo, kwa kuwa Yeye hana kikomo.

⁵⁶ Kwa hiyo kama Yeye hana kikomo, Yeye alijua mwisho tangu mwanzo. Na hiyo ndiyo sababu angeweza kubashiri mwisho tangu mwanzo, Yeye alijua kwa kuwa Yeye alikuwa ni Mungu. Na kama Yeye si asiye na kikomo, basi Yeye si Mungu. Lakini tunajua Yeye hana kikomo, nasi ni wenye kikomo. Sisi huvuruga mambo sana, na kushawishika sana kwamba tuko sawa, ndipo Mungu kwa nia Yake isiyo na kikomo anapanda tu juu sana juu ya . . . “Mawazo yangu yako juu kuliko mawazo yenu,” alisema Mungu, mnaona. Njia Zake zi juu sana kuliko njia zetu, kwa hiyo lazima tujisalisimishe kwa njia Yake.

⁵⁷ Sasa, tumesikia kila namna ya mambo yanayotukia, tumesikia habari za Eliya, tumesikia juu ya bikira Mariamu kote nchini, na tumesikia kila namna ya mihemko na kila kitu namna hiyo. Ambayo si—siko hapa kuzungumza dhidi ya hayo, niko hapa kusema ya kwamba Malaika yeyote wa Mungu, ama mjumbe yeyote wa Mungu, hana budi kudumu kikamilifu katika Neno la Mungu.

⁵⁸ Katika Biblia ya kale walikuwa na njia ya kujua kama ilikuwa ni kweli au la. Walikuwa katika torati zao za Musa walikuwa na kile walichokiita ukuhani wa Haruni, halafu ukuhani wa Walawi, hasa, naye Haruni alikuwa kuhani mkuu aliyebeba kile kifu-. . . kifuani mwake, mawe ya kila kuzaliwa kwa wale wazee wetu.

⁵⁹ Walikitundika kile kifuko cha kifuani, halafu kikaitwa Urimu na Thumimu, na wakati nabii alipotabiri, kama alienda kwenye Urimu na Thumimu, naye akatoa unabii wake, ama kutoa ndoto yake, wala Nuru za kimbinguni hazikuakisi katika mkusanyiko wa Nuru, basi, sijali ilisikika nzuri jinsi gani, ilikuwa ni ya uongo, waliikataa. Waalimu wote wazuri wanajua hilo, ya kwamba wa—wao walilikataa, ilibidi lishuhudie kwenye Urimu na Thumimu. Na sasa, bila shaka wakati ukuhani huo ulipokoma, basi ukuhani mwingine ulikuja ambao, kwa mfano wa Melkizedeki.

⁶⁰ Sasa, sasa siku hizi hatuna yale mawe ya kuzaliwa ya wale wazee wetu, bali tuna Urimu na Thumimu, na hiyo ni Biblia ya Mungu. Yesu alisema, “Mbingu na nchi zitapita, bali Neno Langu halitapita kamwe.” Na katika Kitabu cha Ufunuo, ambacho ni ufunuo wa Yesu Kristo, Alisema, “Kama mtu yeyote ataongeza, ama kuondoa Kwake, huyo ataondolewa, sehemu yake, kutoka katika Kitabu cha Uzima.” *Hiki* Ndicho Urimu na Thumimu.

⁶¹ Joseph Smith alikutana na malaika, halikuwa la Kimaandiko. Sasa, kama malaika yeyote, ama chochote

ambacho ni kinyume na Neno la Mungu, *Hiki* ndicho ufunuo mkamilifu wa Yesu Kristo, kwa hiyo basi dumu Nacho.

⁶² Ndipo Yesu akijitambulisha Mwenyewe kwa ndugu Zake kwa kuzungumza na Simoni, na kumwambia yeye alikuwa ni nani na kwamba baba yake alikuwa ni nani, Simoni alitambua, mara moja, ya kwamba Yeye alikuwa ndiye Masihi. Unaamini ya kwamba Mungu, kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, alijua ya kwamba jambo hilo lingetukia namna hiyo? Yesu alisema hivyo, Yeye aliwajua kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, kwa hiyo, naye Mungu alikuwa amewaita.

⁶³ Sasa, wakati Nathanaeli alipokuja, alikuwa pia, kama nilivyomsikia huyu ndugu hapa akizungumza dakika chache zilizopita, kwamba lilitibitishwa, naye Nathanaeli akiwa ni mtu wa Kimaandiko, alijua ya kwamba huyo alikuwa ndiye Masihi, kile Masihi angefanya. Yule mwanamke kisimani, kama alivyolirejea. Mara ngapi zaidi? Zakayo juu mtini, akijificha kutoka Kwake. Akasimama moja kwa moja chini ya mti, akasema, “Zakayo shuka chini; ninaenda nyumbani pamoja nawe kwa chakula cha kutwa.” Bartimayo kipofu akishuka kwenye umati, huku wakimtupia Yeye vitu, na kupiga mayowe, na kumdhihaki, hata hivyo imani yake ilimsimamisha, na si kumsimamisha tu, bali ilimponya huyo mtu. Mwanamke mmoja aligusa upindo wa vazi Lake, kisha akaenda zake na kuketi chini, Yeye akasema, “Mtu fulani amenigusa.” Ndipo huyo mtume akamkemea kwa kusema Neno kama hilo. Akaangalia kote kwenye kusanyiko mpaka akamwona mwanamke huyo, na kumwambia juu ya kutokwa kwake na damu na kusema imani yake ilikuwa imemwokoa. Mnaona? Ilikuwa ni kamilifu, ishara ya Masihi, nao wakakataa kuitambua.

⁶⁴ Sasa, tetesi langu ni, ni hili kwenye Maandiko, kwamba Yeye—Yeye alifanya ishara hizo mbele ya Myahudi na Msamaria pia, bali si kwa Mataifa, hata mara moja, kwa sababu Mataifa hawakuwa wakimtazamia Masihi yeyote. Lakini je, sisi Wakristo wa Mataifa, usiku wa leo, tunamtazamia Masihi? Yeye alituahidi katika Luka, alisema kwamba hapo tulipoona ishara ya Sodoma, hivyo ndivyo ingekuwa katika kuja kwa Mwana wa Adamu. Mnakumbuka hilo? Jinsi ambavyo Lutu kule chini, yule mwaminio mkwamia mpakani huko chini Sodoma, mfuasi wa kanisa, amechanganyikiwa kabisa na ulimwengu na theolojia yake imechafuka kabisa, lakini kulikuwa na Billy Graham wa kisasa aliyeshuka kwenda kule, nao wakahubiri Injili, na kumtoa Lutu na hao wengine.

⁶⁵ Lakini Ibrahimu alikuwa tayari ametoka. Neno *kanisa* linamaanisha, “walioitwa watoke,” kundi lililoitwa litoke. Kwa maneno mengine, Mungu anaagiza utangano, ulimwengu siku hizi unataka wachanganyaji.

⁶⁶ Wengi wa watu mnapomchagua mchungaji wenu, mnataka

kumchukua mtu atakayechanganya, ambaye atashuka, aende kuogelea ufukoni, ama kunywa, pombe kidogo ya kirafiki pamoja nanyi, ama—ama kufanya maskini mzaha mchafu, ama chochote kile; hilo limezidi sana katika milki za Kiprotestanti siku hizi. Lakini watu wanataka mchanganyaji, bali Mungu anataka watenganishaji. Jitengeni nao, msifungwe nira pamoja na kutokuamini. Hiyo ndiyo njia ya Mungu ya kufanya hilo, ulimwengu una dhana tofauti.

⁶⁷ Sasa, tunapoangalia mbali zaidi katika Neno, tunaona ya kwamba Kanisa lililoitwa litoke, Wateule, kulikuwako na Malaika aliyenena nao na kuwapa ishara. Halafu kulikuwa na Mtu wa kigeni aliyeishi katika mwili, ambaye Ibrahimu baadaye alimwita Elohimu, Mungu Mwenyezi. Na kwa hiyo akaona ya kwamba Mtu huyu alikuwa ameketi, alikuwa ameelekeza mgongo Wake kwenye hema. Na m—mlango tu kabla ya huu Mungu alikuwa amekutana na Ibrahimu na kumpa jina kutoka kwa *Abramu* likawa *Ibrahimu*, *Sarai* likawa *Sara*, na, “binti mfalme,” Naye akawaita wote wawili kwa jina lao la kikuhani, ama walilopewa na Mungu. *Elohimu*, H-e-m, akichukua sehemu ya jina Lake, *Ibrahimu*, kutoka kwa Abram, *himu*, sehemu ya Jina la Mungu, kwa sababu alikuwa awe, pia, baba, kwa uzao, wa mataifa mengi, baba wa mataifa.

⁶⁸ Sasa, m—mnaona kilichotukia pale, sasa, yule Malaika akiwa ameelekeza mgongo Wake kwenye hema, alisema, “Yu wapi Sara, mkeo?”

Alijuaje jina lake lilikuwa Sara? Alijuaje alikuwa ameo? Tena alijuaje mambo haya yote?

Kasema, “Yuko kwenye hema nyuma Yako.”

⁶⁹ Naye akasema, “Kwa muhula wake nitakurudia wakati huu huu mwakani.” Ndipo Sara akacheke moyoni mwake, alipofanya hivyo, huyo Malaika akasema, “Kwa nini akacheke akisema moyoni mwake kwamba ‘Sitaweza kufanya jambo hili, nami ni mzee sana,’ na kadhalika?” Alijuaje hilo?

⁷⁰ Sasa, Yesu kwa udhahiri... Sasa sikilizeni kwa makini, msilikose, na mwe na kicho tu mwezavyo. Angalieni, ahadi hiyo ilifanywa ipate tu kutukia tena katika Kuja kwa Bwana. Mnaona? Sasa, Yesu akieleweka vibaya, walisema nini walipomwona akifanya ishara Zake za Masihi? Walisema, “Yeye ni Beelzebuli.”

⁷¹ Vema sasa, tunajua ya kwamba Beelzebuli alikuwa ni ibilisi, alikuwa mkuu wa pepo. Basi vinginevyo, walimwita Yesu katika kutambua mawazo yao mioyoni mwao, m—mpiga ramli, ama msoma mawazo, ama kitu kama hicho, ambapo tunajua ya kwamba hicho ni cha ibilisi, bila shaka. Na ni—ni kitu kilichopotoshwa, kitu ambacho kimekuwa halisi, kikapotoshwa.

⁷² Ibilisi hawezi kuumba, ibilisi hupotosha tu kile Mungu alichoumba; kuna Muumba mmoja tu, huyo ni Mungu. Uongo

ni nini? Ni ukweli ulioelezewa vibaya. Mwanamke m—mwovu ni nini? Ni mwanamke mzuri ambaye amepotoshwa. Mnaona? Chochote kilichopotoshwa ni cha ibilisi, chochote katika hali yake ya asili ni cha Mungu. Mnaona? Mungu ndiye Muumba pekee. Wala ibilisi hawezi kuumba, hana budi kupotosha kile Mungu alichoumba. Weka hilo niani mwako.

⁷³ Sasa, walimwita Roho wa Mungu, aliyekuwa akifanya ishara hizi kuu kuthibitisha ya kwamba Yeye alikuwa ni Masihi, walimwita huyo pepo mchafu. Naye Yesu alisema ya kwamba “Nitawasamehe jambo hili, lakini wakati Roho Mtakatifu atakapokuja kufanya jambo lile lile, neno moja dhidi Yake halitasamehewa kamwe katika ulimwengu huu, wala katika ulimwengu ujao.” Angalieni jinsi lilivyo kali!

⁷⁴ Sasa, kabla hukumu haijapiga, rehema huja kwanza. Halafu baada ya rehema, basi hakuna... Ukiikataa rehema kuna kitu kimoja tu kilichosalia, hicho ni hukumu. Hukumu hufuata rehema ikiisha kukataliwa. Walimkataa Kristo, hukumu ikafuata; waliwakataa manabii, hukumu ikafuata; na ingawa inaniumiza, kama raia wa Marekani, lazima niseme ya kwamba taifa hili limeikataa rehema, kwa hiyo liko tayari kwa hukumu ya Kiungu ya Mungu.

⁷⁵ Angalieni kile kimeenda kwa taifa hili, mambo ya kila namna, watu mashuhuri kama wale nilionena habari zao dakika chache zilizopita Charles Fuller, Billy Graham, Jack Shuler, Oral Roberts, Tommy Hicks, T. L. Osborn, watu mashuhuri wamevuka taifa hili wakilitikisa, nalo linaendelea kuzama katika dhambi, likisonga mbele moja kwa moja. Baadhi yao watashawishiwa na—na huduma ya watu hawa mashuhuri, nao wataingia na kujiunga na kanisa, kisha watoke moja kwa moja na kuishi jinsi walivyoishi daima. Unapolikiri Jina la Yesu Kristo, achana na dhambi zote, “Kila mtu aliitaye Jina la Yesu Kristo,” Maandiko yanasema, “na aache dhambi.” Lakini tunafanya nini?

⁷⁶ *Dhambi* ni nini? “Kutokuamini.” Kuna dhambi moja tu: kutokuamini. Unafanya uzinzi, unavuta sigara, unalaani, unakunywa pombe, kwa sababu wewe ni asiyeamini. Kama ulikuwa ni mwaminio, usingefanya hivyo, mambo hayo ni sifa za kutokuamini. Mwaminio wa kweli ana msingi thabiti, imara juu ya Kristo, na hakuna kitu kitakachomtikisa. Lakini kwa sababu unayumbayumba, unaelekea upande mmoja, hiyo ndiyo sababu mambo haya yanatendeka maishani mwako. Imani ya kweli isiyoghoshiwa itakushikilia salama msalabani, itakushikilia.

⁷⁷ Sasa, Yeye aliwakemea na kuwaambia, kwa sababu walifanya hivi, Yeye akaanza ku sema (Nami ninashuka kwenye somo langu sasa.) kwamba Malkia wa Kusini atasimama na kukihukumu hicho kizazi. Walikuwa wamemwambia ya kwamba Yeye alikuwa Beelzebuli vifungu vichache tu nyuma ya hiki. Naye alikuwa amewakemea kwa kutokuamini

kwao, alikuwa amewaambia ya kwamba walikuwa na siku, bali walikuwa wameikataa. Yeye alisema wakati mmoja, “Yerusalem, Yerusalem, ni mara ngapi nimetaka kuwakusanya pamoja kama vile kuku awafunikavyo vifaranga vyake, lakini hamkutaka! Sasa mmeachwa.”

⁷⁸ Nami ninaamini ya kwamba Roho Mtakatifu mkuu mioyoni mwa wanaume na wanawake huku Marekani ambao ni Wakristo, wanaweza kumsikia akilia, “Marekani kuu, Marekani, ni mara ngapi ningewapa uamsho, ni mara ngapi, vema, ningewakusanya pamoja, lakini hamkutaka! Mnayapenda mambo ya ulimwengu kuliko kuyapenda mambo ya Mungu, kwa hiyo haya basi.” Ndipo hakuna kitu kilichosalia, ila hukumu ya Kiungu itabidi ishuke, utengano na Mungu.

⁷⁹ Sasa, tunaona ya kwamba katika vizazi vyote Mungu amekuwa na karama. Kila kizazi, kote katika Biblia, kwa kuwa nina Maandiko mengi hapa ambayo ningeweza kuyarejea hapa kwamba—kwamba katika nyakati mbalimbali kwamba Mungu amekuwa na karama za Kiungu.

⁸⁰ Na sasa ninataka kuwaambia makasisi hivi: nawatakeni mniambie, ama mnitajie katika historia, wakati mmoja kwa mwanahistoria yeyote, ama wakati wowote ambapo Mungu aliwahi kumwaga baraka Zake na akawa na uamsho, ila ambapo ishara za Kimbinguni zilifuatana na uamsho huo, kila uamsho. Wamekuwa na uponyaji, na kunena kwa lugha, na madhihirisho ya Roho katika kila uamsho; ni ishara za Mungu. Mungu, alipo Mungu kuna ishara, kwa sababu Mungu ni Mungu atendaye ishara.

⁸¹ Yesu kamwe hakusema, “Je, mliniamini Mimi kwa sababu nilikuwa na mafundisho ya Baba Yangu?” Ati Yeye alisema, “Nisipotenda mafundisho ya Baba Yangu, msiniamini Mimi?” Yeye alisema, “Nisipozitenda *kazi* za Baba Yangu, msiniamini Mimi kama sizifanyi hizo *kazi*.”

⁸² Tumeenda, na kujenga shule, na shule za Biblia, na—na seminari, na kujenga majengo mazuri, lakini hilo bila shaka halikuwa ndilo agizo. Hayo ni sawa, siwezi kusema chochote kiovu dhidi yake, yalitimiza sehemu wao, bali hilo halikuwa ndilo agizo, agizo lilikuwa “Enendeni ulimwenguni kote mkaihubiri Injili.” Kuhubiri Injili kulikuwa ni kudhihirisha nguvu, ilibidi iwe hivyo. Kifungu kinachofuata kinasemaje? “Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Madhihirisho ni . . . Maonyesho ni matendo yaliyotoka katika Neno yakifanywa halisi. Wakati Neno linapohubiriwa, ishara za Neno huthibitisha Neno kwamba ni kweli. Kama halithibitishi, halitoki kwenye moyo wa imani, halitii nanga katika moyo wa imani.

⁸³ Hivi Yesu hakusema ya kwamba wengine walipanda mbegu, nao walipozipanda zilianguka kando ya njia, ndege wakazikusanya? Zingine zikaingia katika udongo wenye mawe,

ndipo utajiri wa nchi ukazisonga, kama miiba, na kadhalika? Na hivi Yeye hakusema zingine zilienda kule na kuzaa mara mia moja? Unaona, lazima kwanza uache Neno lianguke katika imani sahihi. Na katika imani hiyo huzaliwa kile Neno lilichosema, kwa sababu Neno ni Mbegu. Neno la Mungu, papa *hapa*, ni Mbegu ambayo mpanzi hupanda. Na kila mbegu itazaa kwa jinsi yake kama ikiwekwa katika mazingira mazuri na katika hali nzuri, huwezi kuificha, huwezi kuuficha uhai halisi.

⁸⁴ Hebu chukua uhai wa kawaida, uhai wa mimea, acha jua hilo liwe na joto, sasa, kama vile katika nchi yangu, hiyo mbegu ndogo huanguka, kutoka kwenye maua haya, yanakufa, wanafanya msafara wa mazishi, a—anga zinalia machozi makubwa mno ya Oktoba, na kuzizika ardhini, hiyo mbegu inapasuka, nyama inatoka, huo sio mwisho wa hilo ua. Acha tu jua, j-u-a, ambalo lina mamlaka juu ya maisha yote ya mimea, na ndipo linapoanza kuangaza juu ya ardhi na kufikia halijoto fulani, hakuna joto lingine litakalofanya hivyo, hakuna kitu kingine kitakachoiweka rangi hiyo mle ndani ila jua, kwa hiyo acha ifikie halijoto inayofaa, mazingira mazuri, ndipo chembe hiyo ndogo ya uhai iliyofichwa mahali fulani katika huo udongo, itachipuka tena.

⁸⁵ Je, uliwahi kutengeneza njia ya zege, na kuona katika majira ya kuchipua ya mwakani, nyasi zako nyingi ziko wapi? Moja kwa moja ukingoni mwa hiyo njia. Ni kitu gani? Ni mbegu hiyo iliyozikwa chini ya njia hiyo. Na wakati halijoto inapokuwa sawa, msimu unapokuwa sawa, huwezi kuficha uhai, utapenya moja kwa moja, kisha uje uchomoze maskini kichwa chake na kumsifu Mungu, kwa sababu ni uhai, huwezi kuuficha wakati j-u-a linapowaka.

⁸⁶ Hakika tu kama vile j-u-a huleta uhai wa mimea, M-w-a-n-a huleta Uzima wa Milele. Wala huwezi kuuficha, utaangaza, kuna jambo fulani halina budi kutukia. Yesu alisema, “Wakinyamaza, mawe yatapiga kelele mara moja.” Jambo fulani linatukia. Wakati Mungu, Mungu wa Milele, anapoanza kuangaza chini kwa Roho Wake, wale waliokusudiwa Uzima watamtambua, watakuja na kutembea katika Nuru, waishi katika Nuru.

⁸⁷ Naye alisema, “Amin, nawaambia, bado kitambo kidogo, na ulimwengu,” (*Kosmosi*, ambalo linamaanisha “utaratibu wa ulimwengu.”) “hautaniona tena, bali ninyi mtaniona, kwa kuwa Mimi,” *Mimi* ni kiwakilishi nafsi hapo, “Nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari,” kote kote. “Enendeni ulimwenguni *kote*.” Si kwa kizazi hiki tu, ulimwenguni *kote*.

⁸⁸ Ninyi mnaosema kwamba ninii, mnaotaka kusema ya kwamba zile ishara za mitume, ndio pekee waliokuwa na Roho Mtakatifu, ndio tu ambao wangeweza kufanya miujiza, mnawezaje kusoma historia ya Kanisa, na kusema jambo

kama hilo? Vipi kuhusu Polycarp? Vipi kuhusu Ireneo? Vipi kuhusu Mtakatifu Martin? Utafanya nini na watu hao? *Columba*? *Columba*? Hao wote, utafanya nini nao? Mamia ya miaka baadaye wangali wanaponya wagonjwa, wanafufua wafu, walinena kwa lugha, wakatoa pepo, utalifichaje? Maadamu huyo Mwana, M-w-a-n-a, wa Roho Mtakatifu wa Mungu analiangazia Kanisa, ishara na maaajabu yatatokea. Huwezi kulificha, lipo.

⁸⁹ Someni hili pamoja nami, Marko 16: “Enendeni ulimwenguni mwote.” Haijafikia ulimwengu wote bado. “Mkaihubiri Injili,” mdhihirishe nguvu. Kiasi gani? “Kwa kila kiumbe.” Mnaona? “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Umbali gani? Ulimwenguni kote, kila kiumbe. Kamwe huwezi kuuficha. Kamwe hakusema, “Enendeni, mkafundishe Neno.” “Enendeni, mkaihubiri Injili,” onyesheni nguvu za Roho Mtakatifu.

⁹⁰ Sasa, kama hujui Neno, utajuaje ishara hiyo? “Ishara hizi.” Inakubidi kulijua Neno upate kujua kile unachozungumzia. Kama ukilichukua kutoka kwa dhana ya mtu fulani, basi kamwe hukulipata jinsi Petro alivyolipata, ndipo utatoa wazo lako mwenyewe kulihusu. Lakini Yesu alimwambia Petro, “Mwili na damu havikukufunulia hili, bali Baba Yangu aliye Mbinguni. Na juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu; na malango ya kuzimu hayawezi kulishinda.”

⁹¹ Sasa, ili kuona kama ni kweli ama si kweli, rudini mkachukue *Wanzilishi Waliotangulia Nikea*, ama *Baraza La Nikea*, na wa—wanahistoria wa wakati huo, mwone kama katika kila wakati ambapo watu walianini Neno hilo, lilitoa kile hasa lilichosema lingetoa.

⁹² Niliona si muda mrefu uliopita ambapo waliingia kwenye maghala ya Misri wakaona ngano iliyowekwa mle yapata miaka elfu mbili mia tano iliyopita, naam, zaidi ya hiyo, yapata miaka elfu tatu iliyopita, iliyowekwa mle ndani na Yusufu, baadhi ya hiyo ngano ilikuwa imekaa humo kwa miaka hiyo yote, nao wakaipanda ardhini, na ikazaa tena. Haidhuru Injili hii itakaa hapa muda gani, miaka elfu mbili tumekuwa na wenye kudhihaki na wakosoaji, na kusema siku za miujiza zimepita, lakini weka Neno hilo katika aina nzuri ya moyo, Hilo litazaa, tena, kama tu vile *lilivyofanya* mara ya kwanza, kwa sababu ni Neno la Mungu, halina budi kuingia katika mkondo wa imani. Maadamu iliwekwa ghalani haikumaanisha kitu, ilikaa tu mle kama kumbukumbu.

⁹³ Nilishangaa huko Rumi, wana ninii, kwa kweli, misumari kumi na tisa mbalimbali iliyopigiliwa mkononi mwa Yesu. Kila mmoja alisema, “Tunao, kanisa letu linao. Tunao.” Misumari kumi na tisa wanayoweza kuthibitisha, wakati kulikuwako na mitatu tu. Mnaona? Kila mtu anataka msumari.

⁹⁴ Hapa si muda mrefu uliopita nanii mashuhuri (Mnaelewa ninalomaanisha.), mtu mashuhuri alitokea na kipande, “Hiki *hapa* kipande cha ule msalaba asili.”

⁹⁵ Hiyo inaleta tofauti gani? Sijali una misumari mingapi, una vipande vingapi vya msalaba, tunahitaji kutoa Neno hili tena. Sio kuliweka juu ya msalaba, kwenye msumari, bali kwenye mazingira hai ya Roho Mtakatifu, ambayo huleta matokeo. Neno la Mungu, chini ya mazingira mazuri, litazaa kile hasa linachosema litazaa. Halina budi kuwa katika mazingira mazuri hata hivyo, huwezi kuliweka kwenye seminari, ama shule fulani ya Biblia ambayo haiamini katika ishara na maajabu. Kamwe halitafa-. . . Halitapasuka kamwe na kuleta Uhai humo, mazingira hayo ni mabaya, bali huna budi kuliweka katika mazingira mazuri. Mazingira ya aina gani? Mazingira yaliyosalimishwa. Ukae mle mpaka litakapoanza kukua na kupata Uhai, hilo ndilo wazo.

⁹⁶ Kamwe hakusema, “Nikifanya *mafundisho* ya Baba Yangu.” Yeye alisema, “Kama sizitendi *kazi* za Baba Yangu.” Hilo, fundisho, mtu yeyote angeweza kulifundisha, bali hebu tuone kazi zikifanywa.

Unaweza kusema, “Loo, Yeye ni Mungu mkuu.”

⁹⁷ Hakika. Tunaenda kwenye shule za Biblia, si kwamba ninazihukumu, lakini ninajaribu kuninii. . . Natumaini hamnielewi vibaya, sizihukumu shule za Biblia, bali ninazihukumu, kile mnachosema kwamba mna—mnafundisha mambo haya, kisha mnavunjilia mbali msingi wote mpate kusema ilikuwa katika wakati mwingine.

⁹⁸ Ni kama tu kumpa kurumbizi wako vitamini upate kumfanyizia mabawa mazuri, yenye nguvu, kisha unamweka kizimbani. Inaleta faida gani kufanya hivyo? Kwa nini uimarisha mbawa zake kama utamfungia kizimbani? Kile kanisa linachohitaji siku hizi ni kufunguliwa kwa vizuizi hivi vinavyowazuia, na baadhi ya vitamini za Kipentekoste, za Roho Mtakatifu zikimiminwa tena kanisani, ndipo zitabadilisha mazingira. Hiyo ni kweli. Yataanguliwa, yatazaa tai badala ya kuku. Kuku ni, yeye ni ndege, lakini yeye ni ndugu wa kambo, hajui lolote kuhusu mambo ya mbinguni, hajui maana ya kuwa huko juu.

⁹⁹ Moja ya mandhari ya kusikitisha sana niliyopata kuona ilikuwa, nilishuka kwenda kwenye kizimba wakati mmoja, mimi na mtoto wangu Sarah, tulikuwa tukitembea huko, na kulikuwako na ninii, nikasikia kelele na ilikuwa ni tai mkubwa, mtu fulani alikuwa amemnasa, naye alikuwa tu amenyonyoa manyoya yote kutoka kichwani mwake na nchani mwa mbawa zake. Naye angerudi nyuma upande wa pili wa hicho kizimba, naye angekuja akipigapiga mabawa, na angegongesha kichwa chake kwake, huku mbawa zake na manyoya yakiruka,

angeanguka kifudufudi. Nilimwona amelala pale, na hayo macho makubwa ya kijivu yakiangalia kote. Kwa nini? Alikuwa ndege wa mbinguni, anaishi mbinguni, huko ndiko moyo wake uliko. Lakini kwa ujanja wa mwanadamu, alikuwa amemnasa, na kumweka katika kizimba hiki. Naye alikuwa akijaribu kujigongesha atoke kwa nguvu zake mwenyewe, kujigongesha moja kwa moja kwenye ukuta.

¹⁰⁰ Nikawaza, “Hilo ni la kusikitisha!” Niliondoka hapo karibu nikilia. Nikawaza, “Laiti wanguenzi huyo.” Ninachukia kuona kitu chochote kimefungiwa kizimbani.

¹⁰¹ Ninachukia kuona kanisa limefungiwa kizimbani, naam, ukijigongesha tu hata kufa, na kadhalika, pamoja na kila namna ya milo ya supu, na milo ya kutwa, na matabaka, na vyama, na mambo kama hayo. Jamani, hukuzaliwa kuwa hivyo, la, la.

¹⁰² Ndipo nikamwona maskini jamaa huyo, nikawaza, “Laiti ningaliweza tu...” Nikawaza, “Vema, hilo ni tamasha la kusikitisha.”

Sarah akasema, “Baba, maskini ndege yule!”

Nikasema, “Naam, Mpenzi.”

Kasema, “Kwa nini anagongesha kichwa chake na...?”

Nikasema, “Anajaribu kutoka kwenye hizo fito.”

Kasema, “Ni kitu gani kinachomfanya atake kutoka...? Kwa nini asiketi tu chini na kuridhika?”

¹⁰³ Nikasema, “Hawezi. Unaona, Kipenzi, asili yake ni *huko* juu, huko ndiko anakopaswa kuwa. Mabawa hayo makubwa alipewa ili kujishikilia huko juu hewani, kuangalia chini, kuruka juu.”

¹⁰⁴ Nami nikageuka kutoka hapo, nikawaza, “Hilo ni jambo la kusikitisha, bali ninajua jambo la kusikitisha zaidi, kuona kanisa linalojiita kanisa la Mungu, kanisa la Yesu Kristo, limefungiwa kwenye kizimba, wakati, kwa kweli, wanaweza kusoma Biblia na kugundua kwamba hawakuzaliwa wawe kuku waliofungiwa kwenye kitalu, wanadhaniwa kuwa ni tai wanaoweza kuweka mbawa zao katika Upepo Wenye nguvu Unaoenda kasi unaoshuka. Sio lazima wapigepige mabawa, wanajua tu jinsi ya kushikilia mabawa yao na kuruka juu mahali ambapo mambo yote yanawezekana, kuingia mahali panapowatoa kwenye mahali hapa pa kufungiwa tunamokaa, ‘Siku za miujiza zimepita, hakuna kitu kama uponyaji wa Kiungu, hakuna Roho Mtakatifu.’” Loo, inasikitisha! Unaweza kufanya nini?

¹⁰⁵ Sasa, Yesu akizungumza nao, Yeye aliwapa ishara fulani, na kwa kuwa wakati wangu karibu umekwisha, ningetaka kurejea kwenye baadhi ya ishara hizo. Angalieni hapa, Yeye alisema, kifungu kimoja tu nyuma yake, “Kama zile siku... Kama ilivyokuwa katika siku za Yona, nabii...”

¹⁰⁶ Mungu katika vizazi vyote amekuwa na ishara na maajabu, amekuwa na watumishi aliowashughulikia, wakati mwingine mmoja tu. Mlijua hilo? Alishuka chini katika siku za Nuhu kwa mmoja. Na Yeye—Yeye hufikia mfano, pia alisema hivyo katika kule kuja kwa Mwana wa Adamu, na kadhalika. Alishuka mpaka mahali...bali daima amekuwa na mtumishi Wake. Sasa sikilizeni kwa makini, katika dakika chache zijazo sasa. Nafikiri, hasa, nina dakika kumi na tano niwe kwenye wakati.

¹⁰⁷ Angalieni, daima, wakati Mungu alipowatuma watumishi Wake na kuwatumia watumishi Wake karama Zake, kama watu hao waliamini karama hizo, ilikuwa ni yubile nzuri sana kwa hao watu, lakini kama walizikataa ishara na karama alizowapa, daima iliishia katika machafuko (Sasa, mwulize kasisi yeyote umtakaye, ama mwanahistoria yeyote, ambapo ninajua baadhi ya wanahistoria bora sana niwajua wameketi mbele yetu, nimekuwa tu nikizungumza nao.), na hiyo ni kweli, daima wanashindwa, wanapokosa kumtambua Mungu, na karama Zake, ishara Yake. Mungu siku zote ameninii...Aendako Mungu, daima kuna ishara na maajabu. Da-...Aliahidi jambo hilo. "Ishara hizi zitafuata," si *labda*, *zitafuluata*. Uh-huh. Sasa, daima imekuwa hivyo, imetabiriwa kuwa ingekuwa.

¹⁰⁸ Sasa angalieni, katika...Yeye alinena nao kuhusu siku za Yona. Alikuwa akiwakemea kwa sababu walikosa kuiona ishara Yake ya Masihi, lakini yule mwanamke kisimani aliitambua, sivyo? Akasema...

Kasema, "Nenda kamwite mumeo."

Kasema, "Sina yeyote."

Kasema, "Hiyo ni kweli. Umekuwa na watano, na yule unayeishi naye sasa siye mume wako."

¹⁰⁹ Akasema, "Bwana, naona ya kuwa Wewe ni Nabii. Sasa, tunajua ajapo Masihi, hii itakuwa ni ishara ya Kimasihi. Tunajua hii ndiyo, Masihi atafanya hivi. Lakini u nani Nani Wewe?"

Yesu alisema, "Mimi Ndiye."

¹¹⁰ Ndipo akakimbia mjini, na kusema, "Njoni, mwone Mtu Ambaye ameniambia mambo niliyofanya. Haimkini huyo kuwa ndiye Masihi? Si hivyo ndivyo Masihi anavyopaswa kuwa?" Ndipo watu wa mji huo wakamwamini Yesu kwa sababu ya neno la huyo mwanamke. Mnaliona?

¹¹¹ Sasa, Yesu alikuwa pale akifanya mambo hayo, nao walikuwa wamemkataa. Kwa hiyo akasema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Yona," Yona.

¹¹² Kila mtu daima alimdhihaki Yona, nitamtetea Yona. Yona alikuwa na sifa nyingi kuliko watu wanavyompa. Wengi wao wanasema, "Loo, yeye ni maskini aliyerudi nyuma."

¹¹³ La, hakuwa, “Hatua za mwenye haki zinaongozwa na Bwana,” naye Yona alikuwa ni nabii. Mungu alifanya hivyo makusudi, akamwacha aingie meli hiyo ya kwenda Tarshishi badala ya Ninawi. Sikuzote nilimhurumia wakati alipokuwa katika tumbo la huyo nyangumi.

¹¹⁴ Mnajua baadhi ya watu daima huangalia dalili zao, wakisema, “Angalia mkono wangu. Niliombewa, hauna afueni.”

Kamwe hautakuwa, namna hiyo. Huangalii mkono wako, unaangalia ahadi. Unaona?

¹¹⁵ Nilimwombea mvulana fulani hapa miaka michache iliyopita. Maskini baba na mama walikuja kunisihi nimwombe, alikuwa na dondakoo jeusi, nao moyo, ulishuka sana mpaka kadiogramu ikaonyesha kwamba ulikuwa umekwisha kabisa. Nao wakanifanya nivae kama Ku Klux Klan, daktari alinifanya, apate kuniingiza mle ndani. Huyu Daktari alikuwa Mkatoliki, wala asingeniruhusu niingie, maana nimeoa na nilikuwa na watoto, nami nikasema, “Daktari, ungemruhusu kasisi aingie mle ndani kumpa kaida za mwisho?”

Akasema, “Naam, lakini wewe si kasisi.” Kasema, “Kasisi asingekuwa na watoto wa kuwaendea.”

Nikasema, “Lakini yeye huketi katika kibanda cha maungamo.”

Akasema, “Endelea.” Naye akaniacha niende.

¹¹⁶ Kwa hiyo nikaingia mle ndani, naye maskini huyo baba na mama wakasimama upande mmoja, na kusema, “Ndugu Branham, yote tunayotaka ufanye ni kusema neno.” Nikaingia mle ndani, na kuomba, na kumwekea mikono huyo mtoto mchanga, mimi, ama, mvulana huyo, alikuwa na umri wa kama miaka kumi na miwili, Nikasema, “Baba wa Mbinguni, hii ni ahadi, hii ndiyo uliyoahidi: Ninaweka mikono juu ya kijana huyu sasa, na ninaomba kwa ajili ya uhai wake kwa sababu Wewe uliahidi jambo hilo. Watu hawa wanaamini, nao wakanituma nije hapa. Haya ndiyo yote ninayojua kufanya, ni kumwekea mikono, kwa sababu Wewe ulisema, ‘Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.’” Nikamwekea mikono, nikaondoka, nikasema, “Sasa, Bwana awabariki.”

Mara baba akamshika mama, na kusema, “Loo, mpenzi, si ni ajabu! Ni...” Huyu mvulana kamwe hakuonyesha ninii moja...?...

¹¹⁷ Naye maskini nesi, baada ya baba na mama, huku wakilia tu, wakikumbatiana, mmoja na mwenzake, wakishangilia kwa sababu huyo mvulana alikuwa mzima, mnaona, vema, mvulana huyo hakuwa amebadilika hata kidogo, ndipo maskini huyo nesi akasema—akasema, “Mbona, bwana, unatambua hii ni nini?” Kasema, “Unaweza je kutenda hivyo na mtoto wako yuafa?”

Kasema, “Mtoto wangu hafi, mtoto wangu yu hai, ataishi.

¹¹⁸ Akasema, “Vema,” akasema, “bwana, nataka kukwambia jambo fulani.” Kasema, “Unaona kile kitu cha umeme cha kupima moyo?” Kasema, sielewi alichosema, bali alisema, “Wakati mkono huo,” ama chochote kilichokuwa, “uliposhuka mpaka *hapa* chini, haujawahi kujulikana katika historia ya matibabu kurudi tena.” Kasema, “Huyo mvulana yuafa.” Kasema, “Moyo wake unapiga mara *kadhaa* sasa, kwa dakika,” kasema, “hautarudi tena. Isitoshe ugonjwa huo umemweka katika hali mbaya sana, na u—umeenea sana hata hakuna kitu kinachoweza kufanywa, mvulana huyu anakufa.”

¹¹⁹ Wala kamwe sitamsahau maskini baba huyo hodari, alimchukua maskini nesi huyo na kumkumbatia, alikuwa ni mtoto tu, naye akasema, “Angalia, mama,” kasema, “sikulaumu, wewe ni—wewe ni...umefunzwa kuangalia chati hiyo.” Kasema, “Hayo tu, hayo ndiyo unayojua. Umesomeshwa na kuambiwa na historia na madaktari wenu, na kadhalika, kwamba...” Kasema, “Unaangalia hiyo chati, hiyo tu ndiyo unayojua,” bali kasema, “Ninaitazama ahadi.”

¹²⁰ Mnajua mvulana huyo ni nani? Ni Bob Bosworth huko Afrika Kusini usiku wa leo, akihubiri Injili, mtu aliyeoa aliye na familia. Hiyo ni kweli. Kwa nini? Inategemea kile unachoangalia. Unaona? Wewe mwangalie Mungu, angalia ahadi Yake.

¹²¹ Sasa, kama...Sikuzote nimewazia mtu fulani alikuwa na kisa kizuri cha dalili na alikuwa na haki, ilikuwa ni Yona. Sasa, alikuwa katika tumbo la nyangumi kwenye bahari yenye dhoruba, mikono na miguu imefungwa nyuma yake, amelala katika tumbo la nyangumi lililojaa matapiko. Sasa, kama aliangalia *huku*, ilikuwa ni tumbo la nyangumi, *huko* ilikuwa ni tumbo la nyangumi, *huko* ilikuwa ni tumbo la nyangumi, kila mahali alipoangalia ilikuwa ni tumbo la nyangumi. Sasa, sidhani kuna mtu yeyote hapa aliye mbaya hivyo. Mnaona? Wako—wako tu katika ninii...Hiyo—hiyo ni hali mbaya sana kuwamo.

¹²² Lakini mnajua yale aliyosema? Alisema, “Huo ni ubatili wa uwongo, sitauangalia.” Lakini akasema, “Mara nyingine tena nitalitazama hekalu Lako takatifu.”

¹²³ Wakati Sulemani alipoliweka wakfu hekalu aliomba, wakati Nguzo hiyo ya Moto ilipoingia, ule moshi nyuma Yake, kisha ikashuka nyuma ya mahali patakatifu, aliweka wakfu hekalu, na kusema, “Bwana, kama watoto Wako wakiwa katika shida mahali popote, nao watalitazama hekalu hili takatifu, na kuomba, basi sikia kutoka Mbinguni.” Naye aliamini hilo lingekuwa sawa, kwa sababu Sulemani alikuwa ni mtumishi wa Mungu. Naye akaomba, naye Mungu alifanya nini? Sasa, nisingeweza kuwaambia kisayansi, huenda aliweka tangi la oksijeni kule chini, sijui alilofanya. Lakini alimweka nabii huyo hai kwa siku tatu mchana na usiku katika tumbo la nyangumi huyo. Hiyo ni kweli?

124 Vema sasa, kama atafanya hivyo kwa hali *hizo*, kwamba imani katika m—mtu ambaye hatimaye alirudi nyuma, Sulemani alirudi nyuma, wake zake walimwondoa kwa Mungu, kama alikuwa na matumaini kiasi hicho katika maombi ya Sulemani, katika hali kama hiyo, chini ya hali *hizo*, ni zaidi sana vipi inatupasa usiku wa leo, chini ya hali *hizi*, kuangalia mbali na dalili zetu, kwenye mkono wa kuume wa Mungu, ambapo Yesu amesimama na Damu Yake Mwenyewe, akituombea tunapokiri?

125 “Mara nyingine tena, Bwana, angalia hekalu Lako takatifu, ambapo Mwana wa Mungu aliye hai aliyefufuka amesimama na nguo Zake Mwenyewe zilizolowa damu mbele za Mungu kufanya maombezi, atuombe kama Kuhani Mkuu juu ya yale tunayokiri kwamba Yeye amefanya.” Jamani, angalieni yale Mungu aliyofanya.

126 Nilisoma hadithi moja si muda mrefu uliopita, huenda nikaiingiza hapa kama hamjali. Angalieni, mnajua, watu wote wa Ninawi, lilikuwa ni jiji kubwa, karibu sana na ukubwa wa St. Louis hapa juu, vema, tunajua ya kwamba walishuka kwenda kule, na wote walikuwa wamemwacha Mungu, nao walikuwa makafiri, nao walikuwa wakiabudu sanamu. Na kazi yao kule kando ya bahari, bila shaka, walikuwa ni wavuvi. Watu wote walitoka wakaenda mapema asubuhi, maelfu ya mitumbwi baharini, nao wakavuta samaki. Lilikuwa ni jambo muhimu sana, nao waliuza samaki nje ya nchi, na kadhalika, wapate riziki.

127 Na sasa, mungu wa bahari alikuwa nyangumi. Basi wazieni tu juu ya watu wote huko nje kwenye—kwenye, huko nje kwenye mashua zao za samaki, huko nje wakivua samaki, na wanawake wote na watoto wamesimama ukingoni wakiwangojea waume wao kuingia, wakileta samaki, na waliowakamata, na kadhalika. Na muda si muda mwajua, mungu wa bahari anainuka, nyangumi, anakimbilia ufukoni, anatoa ulimi wake kama ubao wa kushukia, ndipo nabii anakuja akitembea moja kwa moja kutoka kinywani mwake. Hakika. Si ajabu walitubu. Naam, bwana. Hakika. Walitubu kwa sababu mungu alikuwa amemtoa nabii, nao wakasikiliza maneno yake, kwa sababu alikuja kule kwa njia ya kimbinguni.

128 Basi angalieni, Yesu alisema, ya kwamba kizazi kiovu na cha zinaa kinatafuta ishara. Je, alisema hivyo? Hili papa hapa, soma kifungu hiki: “Kizazi kiovu na cha zinaa chatafuta ishara, wala hawatapokea ishara yoyote, isipokuwa kama vile nabii Yona alivyokuwa katika tumbo la nyangumi siku tatu mchana na usiku, Mwana wa Adamu hana budi kuwa katika moyo wa nchi siku tatu mchana na usiku.” Sasa, ni ishara gani ambayo kizazi kiovu na cha zinaa kingepokea? Ishara ya ufufuo.

129 Vema sasa, niambieni, ni lini tuliwahi kuwa na kizazi kiovu zaidi na cha zinaa? Wakati wapotovu walio hapa California

wakiongezeka asilimia ishirini hadi thelathini kila mwaka! Wakati katika serikali yetu wenyewe wanadai kwamba asilimia thelathini na tano au arobaini ni walawiti! “Kama ilivyokuwa katika Sodoma...” Niambieni wakati tulipopata kuwa na wengine waovu zaidi, mbona, watu hufanya mambo ambayo watu wa kale wasingewazia kuyafanya, ile adhabu kali.

¹³⁰ Waovu, wasioamini, wasioongoka, kila mawazo mabaya katika moyo wa mwanadamu, kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, hicho ndicho kizazi alichokuwa akinena habari zake. Kizazi kiovu na cha zinaa kitapokea ishara ya namna gani? Ishara ya Yesu aliyefufuka, ishara ya ufufuo, wangeipokea. Sasa, Yeye anasema hivyo papa hapa katika Maandiko.

¹³¹ Sasa, ndipo anashuka kwenye fungu la kumalizia, “Na kama ilivyokuwa katika siku za Sulemani, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu. Maana katika siku za Sulemani malkia wa kusini alikuja kutoka pande za mwisho za ulimwengu unaojulikana kusikia hekima ya Sulemani.”

¹³² Sasa, hebu tumchukue Sulemani katika wakati wake, kwa muda kidogo tu. Sulemani alikuwa mtu mashuhuri wa Mungu, ambaye Mungu alimpa karama. Karama yake ilikuwa ni upambanuzi. Ni wangapi wanaojua hilo? Hakika, ilikuwa. Vema. Basi angalia Israeli yote. Ni walimu wangapi wa Biblia hapa wanaojua ya kwamba huo ulikuwa ndio wakati wa ufanisi wa Israeli? Hakika, ulikuwa. Walijenga hekalu, walifanya mambo makubwa zaidi, hapakuwapo na vita wala chochote kile. Vema hakika. Kwa nini? Wote walikuwa na nia moja, wakitoa sifa kwa yale Mungu aliyowafanyia, kila mmoja wao aliiunga mkono karama hiyo kuu. Nao Israeli walikuwa na amani na mataifa mengine yote.

¹³³ Hebu nisisimama hapa kwa dakika moja. Kama Marekani ingechukua sayansi yake na kujaribu kutafuta utafiti wa kuponya kansa, ama jambo fulani ambalo lingemsaidia mtu fulani, badala ya kujaribu kuninii, ama, hapa nitabadilisha hilo: Kama Marekani ingeigeukia karama yake kutoka kwa Mungu, na kupokea karama ya Mungu iliyo katika taifa hili sasa, isingewabidi kujenga mabanda ya mabomu na kadhalika, ya kujisetiri, ulimwengu mzima ungeliogopa taifa hili. Kuna silaha moja tu dhidi ya ukomunisti, na hiyo ni Kristo. Kristo ndiye ukomunisti unamwogopa.

¹³⁴ Nilikuwa nimesimama kule Urusi, ama, si Urusi, bali Ufini, wakati yule mvulana mdogo, mlilisoma kwenye magazeti, na kadhalika, wakati mvulana huyo mdogo alipofufuliwa kutoka kwa wafu. Na huko, unapokuwa Urusi, wakati ukiwa umbali wa maili arobaini kutoka mahali ulipozaliwa, inakubidi kuwa na visa kuonyesha ya kwamba una shughuli ya kuwa umbali wa maili arobaini kutoka mahali ulipozaliwa. Basi wakati hiyo ilipotangazwa kwenye redio siku hiyo kwamba mvulana huyo

mdogo alikuwa amefufuka kutoka kwa wafu, kutoka kulala pale...

¹³⁵ Wengi wenu ninyi watu mnaoketi papa hapa mlioandika hayo katika Biblia yenu miaka miwili kabla jambo hilo kutukia nilipowaambia, ni wangapi walioko hapa ndani wanaoniambia wamesikia, nami ni—niliwaambia uandike katika Biblia yako ya kwamba kungekuwako na ufufuo wa mvulana mdogo, kwamba ningevuka kupitia magharibi, na yote hayo? Ni wangapi waliopo hapa wanaoikumbuka hadithi hiyo? Inua mkono wako. Angalieni hapo. Mnaona? Kila mahali jengoni. Miaka miwili kabla halijatukia. Hapo yule mvulana mdogo, si ilikuwa vile hasa lilivyosema ingekuwa? Hakika. Mungu daima, Yeye hulifanya kwa njia ifaayo kabisa.

¹³⁶ Sasa, jinsi tu Yeye anavyosema itakuwa, hivyo ndivyo itakavyokuwa. Hiyo ndiyo sababu Neno Lake, wakati Wake, na kila jambo litakuwa kama tu vile Yeye alivyolisema. Haidhuru ni nani asiyeliamini, litakuwa hivyo, kwa vyovyote vile. Mnaona?

¹³⁷ Kwa hiyo nilipokuja hu—huko Messuhalli usiku huo, waliwaingiza kama watu elfu thelathini ndani, kisha kuwafanya watoke nje, ndipo wengine elfu thelathini wangeingia niwazungumzie. Ndipo basi nilipokuwa nikishuka kuja barabarani, hawa hapa maskini hao askari wa Kifini hawakuwa wamenyoa ndevu bado, wavulana tu, kama sita, saba mbele, na sita, saba nyuma. Na hapo walisimama wale wakomunisti, askari wa Kirusi, wamesimama hapo wakipiga saluti hiyo ya Kirusi wakati nikipita, huku machozi yakitiririka mashavuni mwao, mara wakawashika hao askari wa Kifini na kuwakumbatia. Chochote kitakachomfanya Mfini kumkumbatia Mrusi, na Mrusi amkumbatie Mfini kitabadilisha vita na kuvisuluhisha milele. Walisema, “Tutampokea Mungu kama huyu, Mungu aliye na nguvu, Mungu anayeweza kujionyesha Mwenyewe Mungu!”

¹³⁸ Jambo ni kwamba, makanisa yetu walilimimina kwenye chupa likawa chama. Ni zaidi ya chama, ni ubatizo katika Mwi—Mwili wa Yesu Kristo aliye hai, aliye fufuka pamoja na nguvu na ishara na maajabu. Hiyo ni Injili, hiyo ni Kristo, huyo ni Mungu.

¹³⁹ Mwangelie, hakika, Sulemani, kila mtu alimzunguka, kila mtu angesema, “Loo,” kila mtu kwa nia moja, walisema, “loo, njoni, mwone karama kuu ambayo Mungu wetu ametupa. Njoni, mwone karama kuu ambayo Mungu wetu ametupa.”

¹⁴⁰ Mungu anapotupa Karama ya Roho Mtakatifu, hiyo ni Karama yetu, Roho Mtakatifu, Mungu alitutumia Roho Mtakatifu, tunafanya nini? Tunamcheka, tunawaita watakatifu wanaojibingirisha, tunawafukuza watoke pembeni, tunawaambia wanao kichaa, wamerukwa na akili, hawatoki kwenye shule zetu, wao si kitu ila kundi la watu wa lugha. Hiyo ndiyo sababu tunapokea hukumu.

¹⁴¹ Walifanya nini kwenye Siku ya Pentekoste? Hao Wayahudi walifanya nini? Walicheka na kumdhihaki. Walifanya nini miaka michache baadaye? Tito alizingira hayo malango, na kuwaulia humo ndani moja kwa moja, mpaka damu ikatiririka nje ya malango, na kupageuza mahali hapo juu chini, akalibomoa hekalu, wametawanyika tangu wakati huo. Kweli.

¹⁴² Tutapata yayo hayo. Mmeikataa Karama ya Mungu, Roho Mtakatifu, mliweka kupeana mkono, ama barua kutoka kwa kanisa lingine kuchukua mahali Pake. Roho Mtakatifu si kupeana mikono, wala si barua, ni karama ya Mungu pamoja na nguvu zitokazo Juu kuwaonyesha watu. Huyu ni Roho wa Mungu anayeishi ndani yetu, anayeifanya, na kuionyesha, na kuwathibitisha watu kwa ishara na maajabu ya kwamba ni Mungu. Haleluya!

¹⁴³ Ninajua mtaniita mtakatifu anayejibingirisha baada ya hili, lakini, labda mimi ni mmoja. Ninajisikia wa kidini sana sasa hivi, kwa vyovyote vile.

¹⁴⁴ Angalieni, Mungu, madhihirisho, nguvu, akijithibitisha Mwenyewe ya kwamba Yeye ni Mungu. Hayo ni Maandiko, hawezi kukana hilo, ila kwamba ni kweli, karama za upambanuzi.

¹⁴⁵ Sasa, ninii yote...Wazia tu wapitaji wangesema, “Loo, unapaswa kuja kwenye taifa letu, umwone Mungu wetu mkuu, mwenye nguvu. Mbona, Yeye—Yeye hufanya kazi miongoni mwa watu wetu. Yeye—Yeye hufanya ishara kuu na maajabu. Tunaye mfalme aitwaye Sulemani, unapaswa kuona upambanuzi mkuu alio nao mtu huyo. Mbona, ha—haliwaziki.”

¹⁴⁶ Vema, mwajua, imani chanzo chake ni kusikia, sivyo? Kusikia Neno la Mungu. Kwa hiyo, hizo habari zikaenea kote ulimwenguni, kila mahali palisikia kuhusu hili. Nao wote wakaanza kuogopa, kwa sababu, sio kumwogopa Sulemani, bali kumwogopa Mungu, kwa sababu Mungu aliye hai alikuwa akionyesha.

¹⁴⁷ Hatimaye, hizo habari zikafika huko Sheba, chini kabisa, yapata, mamia ya maili huko chini, yapata maili mia tatu chini kusini, chini kabisa, kupitia kwenye Jangwa la Sahara. Ipime kwenye ramani yako uone ilikuwa umbali gani. Sasa, hawakuwa na televisheni siku hizo, na redio, na magazeti, na simu, wao, walisafiri tu kwa—kwa mdomo hadi sikio, nayo misafara ingepitia huko na kuleta habari.

¹⁴⁸ Na kila mtu akishuka kwenda Sheba angemwambia maskini huyo Malkia, “Aisee, inakupasa kwenda huko—huko Palestina, mnajua wana Mungu huko juu aliyewabariki sana hao watu, wote wako na nia moja. Hakuna mzozo wowote miongoni mwao hata kidogo, nao wana ndugu huko juu, wanamwita Sulemani, wamemfanya mfalme. Nao wananiambia ya kwamba Mungu

anamtumia tu kwa kila kitu walicho nacho wanachohitaji, yeye anaweza tu kuwaambia.”

¹⁴⁹ Mnajua, basi imani chanzo chake ni nini? Kulisikia Neno. “Na heri wenye njaa na kiu ya haki, hao watashibishwa.”

¹⁵⁰ Kwa hiyo, maskini huyo malkia akaanza kuona njaa, akawaza, “Unajua, itanibidi kwenda kuona hiyo.” Sasa, mnakumbuka, yeye ana sifa nyingi sana, mwajua, kwa sababu yeye ni Malkia. Kwa hiyo nadhani alisema, “Kabla sijafanya jambo hili sasa, afadhali niende nikamwulize mchungaji wetu kama ninaweza kwenda ama siwezi,” mnaona, “kwa sababu inanibidi kupata ruhusa kutoka kwa dhehebu langu, kwa sababu hilo ni dhehebu lingine.” Mnaona? “Kwa hiyo afadhali niende nikamwulize mchungaji wangu kama ninaweza kwenda, kasisi wangu.”

¹⁵¹ Kwa hiyo ninaweza kumwona akienda pale, na mlinzi mdogo pamoja naye, akasema, “Baba mtakatifu, naomba nipate ruhusa kutoka kwako, kutoka kwa kanisa hili kubwa, takatifu tulilo nalo hapa Sheba, naomba nipate ruhusa kutoka kwako, wana uamsho huko Palestina, naweza kuhudhuria uamsho huo?”

¹⁵² “Upuuzi, binti yangu. Sasa, kama kungekuwa na kitu kama hicho, nimesikia upuuzi huo pia, ni bure, ni kundi tu la watakatifu wanaojibingirisha, ni—ni bure, lakini angalia, kama kungekuwa na nguvu zozote katika mungu yeyote, zingekuwa katika mungu wetu papa hapa. Zingekuja kwa dhehebu letu, zingekuwa ni zetu, kama kuna chochote kwake. Unaona?”

¹⁵³ Loo ndugu, unajua, ibilisi humchukua mtu wake, bali kamwe si roho yake. Hiyo ni kweli. Mungu humchukua Wake, pia, bali kamwe si Roho Wake. Alimchukua Eliya, bali Roho yake ikaja juu ya Elisha, kisha ikaja juu ya Yohana Mbatizaji. Naye akamchukua Mwanawe, Yesu, bali Roho Mtakatifu akarudi Kanisani kufanya kazi zile zile. “Ninii, Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya.” Mnaona, inaendelea kushuka. Naye ibilisi humchukua mtu wake bali kamwe si roho. Hizo roho mbili zingali zinapigana, moja kwa moja.

Sasa, kasema, “La, huwezi kwenda.”

¹⁵⁴ “Vema,” akasema, “sikiliza, unajua, kuna *kitu fulani* chini moyoni mwangu.” Unajua kuna jambo fulani kulihusu, Mungu anapoushika moyo wa mwanadamu, Yeye . . . wanafanya mambo ya kuchekesha. Naam. Kasema, “Lakini unajua nini, nimekuwa na, baba mtakatifu, nina, ama—ama, Askofu mpendwa, Mwangelizi Mkuu, nimekuwa na shauku kubwa sana ya kwenda. Daima nimesikia kuhusu mikutano hiyo, nami ningependa kwenda.”

¹⁵⁵ “Sasa, angalia ewe mtoto, tutakufukuza tu tukutoe kwenye kitabu.” Mnaona? “Tutakuondoa tu, jina lako moja kwa moja kutoka kwenye shirika hili kama ukienda.”

¹⁵⁶ “Vema,” akasema, “lakini angalia, nataka kusema: Sitafanya madhara yoyote, nitarudi moja kwa moja hapa chini bila shaka, mara tu uamsho utakapokwisha, mara nitakapopanda kwenda kule.”

¹⁵⁷ “Lakini huwezi kwenda, nimetoa tangazo hilo, na hivyo ndivyo hao wengine wanavyosema, na hilo ndilo tunalopaswa kushikilia. Sasa, kama kuna kitu kama hicho kinachoendelea, kingekuwa papa hapa pamoja nasi.”

¹⁵⁸ Ninaweza kumwona maskini huyo Malkia, Mungu akitenda kazi moyoni mwake, akajigeuza, akasema, “Nataka kukwambia jambo fulani!” Um-hum! Tunahitaji wengine kama hao. “Nimekuwa katika kitu hiki kwa miaka na miaka, mama yangu alikuwa ndani yake, nyanya yangu alikuwa ndani yake, na yote niliyoona ni lundo la makaratasi, lundo la maandishi, na kuzungumza juu ya mungu fulani, lakini sijaona namna yoyote ya uamsho hata kidogo. Sitaki vitu hivi vilivyokufa, wananiambia wana Mmoja huko juu aliye hai, anayeishi ndani ya watu Wake, na hilo ndilo ninalotaka kuona.” Amina.

¹⁵⁹ Mungu atupe Malkia wengine wa Sheba huku Long Beach. “Ninataka kuona kitu kilicho na Uhai ndani yake. Ninataka kuona kitu ambacho... nimekuwa nikisoma Magombo yote ya ninii ya kale... ya Vitabu vyao huko juu, nao wananiambia ya kwamba Mungu huyo ni Mungu anayejua siri za moyo. Nao wananiambia ya kwamba mtu huyo, Sulemani, huko juu, mchungaji, anaweza tu kufanya mambo haya na ni ajabu sana. Nami ninaenda kuliona.”

“Ukifanya hivyo, nitakufuta tu kwenye kitabu.”

¹⁶⁰ “Vema, afadhali unifutilie mbali sasa hivi, kwa sababu ninaenda.” Ninapenda hilo, um-hum. “Ninaenda, kwa vyovyote vile.” Vema sasa, angalieni, wakati aliponinii, kilichomgharimu.

¹⁶¹ Mnajua, sio rahisi kumjia Kristo. Hiyo ndiyo shida yenu ninyi Wamarekani siku hizi, sisi Wamarekani, kila kitu ni rahisi sana, hakuna mateso, hakuna chochote. Hatujawa na vita, kwa hiyo tunaweza tu kutenda mabaya tutakavyo.

¹⁶² Nilienda Uswisi, nawe unaweza kuwasikia wakipiga kengele, ungefikiri ule Utawala wa Miaka Elfu ulikuwa unaendelea. Hiyo ni kweli. Lakini wanafanya nini? Hata hawaamini ya kwamba Yesu alizaliwa na bikira, wana fundisho la kale la Zwingli, wanaamini ya kwamba Yeye alikuwa ni mwana wa Yusufu. Lakini wanapiga hizo kengele hata ni—ni—nikafikiri ule Utawala wa Miaka Elfu ulikuwa umeanza. Kaniamsha Jumapili moja asubuhi, wala sikujua kilichokuwa kikiendelea, yapata saa moja na nusu.

¹⁶³ Ndipo yakaja yapata mabasi themanini au tisini yenye vioo juu kutoka Ujerumani. Mwajua, Uswisi hawana vita vyovyote, haiwalazimu kuhofu juu ya chochote, wao ni waovu tu na wabinafsi kama Wamarekani walivyo. Nawe unashuka moja

kwa moja kupitia kule, na muda si muda mwajua, umeshuka ku—kuja, Ujerumani ikashuka. Ndipo tulipoenda mkutanoni usiku huo, Ndugu Arganbright aliyeketi hapa, alikuwa papo hapo. Roho Mtakatifu aliwaita nani? Kila mmoja alikuwa ni Mjerumani, Yeye aliwaacha Waswisi wameketi pale pale, pamoja na kengele zao zote, na kadhalika. Mnaona?

¹⁶⁴ Inahitaji mateso. Inakubidi kuchimba. Loo, jamani, laiti mngalijua! Si rahisi, chochote unachokabidhiwa katika sinia, hukifurahii, bila shaka, huwezi kuthamini kile unachopewa.

¹⁶⁵ Mungu alimwambia Musa, akasema, “Nakupa Palestina, nilifagia nyumba zote, na kufunga mapazia, ninyi nyote nendeni moja kwa moja mkaishi mle.” Kama ingalikuwa hivyo, kamwe wasingalifurahia hilo. Yeye alisema, “Nitawapa, imejaa majitu, itawabidi kupigania kila inchi ya njia, lakini kila mahali nyayo za mguu wako zinapokanyaga, hiyo ni milki. Nendeni, mkaimiliki, hakika, kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi.”

¹⁶⁶ Hivyo ndivyo uponyaji wa Kiungu ulivyo, hivyo ndivyo alivyo Roho Mtakatifu, kila kitu unachoweza kutembea nyuma yako, nyayo za miguu ni umilikaji, endelea kutembea, endelea kusonga mbele. Hiyo ndiyo njia. Sogeza tu kidole chako, usingeweza kukisogeza hata kidogo, unasogea *kiasi hicho* leo, unakisogea *kiasi hicho* zaidi kesho, na *kiasi hicho* zaidi kesho yake, endelea tu kusonga, kusonga, kusonga, kusonga. Nyayo za miguu ni umilikaji.

¹⁶⁷ Angalieni, upesi sasa, msichana huyo alikuwa na mengi ya kumkabili. Ilimbidi kufanya nini sasa? Alisema, “Mnajua,” alikuwa na jambo zuri la maana, akasema, “mnajua nitakalofanya?” Akasema, “Nitachukua pesa kidogo niende nazo. Kama ni—kama ni kweli, kama ni kweli, nitaiunga mkono, lakini kama si kweli nitazirudisha moja kwa moja.”

¹⁶⁸ Loo ndugu, je, hilo halingeweza kuwafundisha Wamarekani jambo fulani? Naam, bwana. Kuunga mkono mambo yanayowacheka na kuwadhihaki. Hiyo ni kweli. Vipindi vinavyokucheka na kukuita mtakatifu anayejibingirisha, na hata hivyo unakiunga mkono kwa pesa zako, na mmishenari wenu mwenyewe yuko huko, akiishi kwa sahani mbili zilizojaa wali kwa juma, bila viatu miguuni mwao. Jioneni aibu!

¹⁶⁹ Weka pesa zako kwenye kitu kilicho na Mungu ndani yake na usonge mbele nacho. Si kwa sababu yote yamepambwa, na majengo ya dola milioni sita nyuma yake, na vitu kama hivyo, pamoja na theolojia na kuwapeleka wamishenari wao huko juu na kufanyiwa uchunguzi wa akili na mtaalamu wa akili wa kilimwengu kuona kama wana nguvu za kutosha kiakili kuwa mmishenari. Mungu Ndiye wa kuamua hilo kwa Roho Mtakatifu. Naam, bwana. Hatuhitaji upuuzi huo, tunamhitaji Mungu. Angalieni basi, kwani watu wanaweza kufikia umbali gani? Tunapotea tu.

¹⁷⁰ Sasa, maskini huyo malkia, akasema, “Nitaninii, kama si kweli nitarudisha hizi pesa.” Kwa hiyo akapakia kila namna ya vito, na uvumba, na kila kitu.

¹⁷¹ Sasa, angalieni, jambo lingine, vipi kama angaliwazia... Akiwa na pesa hizi zote ilimbidi kuvuka Jangwa la Sahara, nanyi mwajua, watoto wa Ishmaeli wako huko nje, wote walikuwa ni wanyang’anyi. Vipi kama walishambulia maskini huo msafara wake mdogo, matowashi wachache tu, na wasichana kadhaa pamoja naye, ingekuwa? Mbona, wangalimwibia katika dakika moja na kuchukua pesa zote. Lakini mnajua, ikiwa—ikiwa Mungu anaita moyoni mwako, hujui hofu hata kidogo, endelea tu kusonga mbele, hujali yale mtu mwingine yeyote asemayo, ama chochote kile, unaendelea kusonga mbele wakati unapoona njaa na kiu kwa ajili ya haki.

¹⁷² Kumbukeni, pia, si ajabu Yesu alisema angesimama katika siku za mwisho, na kukihukumu kizazi hiki. Mnajua ilimchukua muda gani kuvuka pale? Inachukua miezi mitatu, siku tisini. Wala hakuwa katika Kadilaki iliyoyoyozwa pia, la, la, alivuka juu ya mgongo wa ngamia kusikia hekima ya Sulemani, naye Yesu akasema, “Aliye mkuu kuliko Sulemani yupo hapa.” Na jambo lile lile hapa: Roho Mtakatifu yuko hapa, na watu hata hawatavuka barabara kumsikiliza. Hiyo ni kweli. “Hapa yupo aliye mkuu kuliko Sulemani.”

¹⁷³ Akafika mahali pale, angalieni wakati alipovuka, kisha akatoka na kuja kwenye nyua za Sulemani. Sasa, ninawazia... Mngeweza kuwazia (nitamfanya raia wa Marekani.), akaingia, “Nitashuka na kuketi chini, kisha nimsikie huyo mtakatifu anayejibingirisha kwa dakika chache tu, kwa sababu jirani hapa, mjakazi wangu aliniambia yanipasa niende, asiposema jambo linalofaa, hasa kabisa, nitasimama moja kwa moja na kuondoka”? Loo, jamani! “Ama atasema kile ninachoamini anapaswa kusema, au sitamsikiliza hata kidogo.”

¹⁷⁴ Hapo ndipo tunaposimama usiku wa leo. Hiyo ni kweli. “Kama akisema jambo moja ambalo mchungaji wangu alisema lilikuwa ni kosa, papo hapo nitasimama tu na kutoka nje.” Mnaona? Sasa, mtasimama pamoja naye, pia, katika Siku ya Hukumu, na ndipo mtahukumiwa pamoja. Mnaona? “Kwa maana hapa yupo aliye mkuu kuliko Sulemani,” Roho Mtakatifu yupo hapa. Mnaona?

¹⁷⁵ Naye akaja siku tisini juu ya mgongo wa ngamia kupitia kwenye mchanga wenye joto, unaowaka moto, kusikia hekima ya Sulemani. Hakuja tu kuingia, aseme, “Nitaingia ndani na nitaona, na kama siipendi vizuri, nitaamka na kutoka nje.” La, alipiga kambi moja kwa moja huko nje uani, akasema, “Nitakaa mpaka nitakaposhawishika. Nitayachukua Maandiko nami nitatafuta kujua,” tayari alikuwa ameyasoma Hayo yote, kile Mungu alichopaswa kuwa, “nami nitajua kama ni kweli.”

¹⁷⁶ Kwa hiyo ninawazia kesho yake asubuhi alijinadhifisha, pamoja na maskini wajakazi wake, kisha akaenda kanisani, ndipo akachukua kiti chake, akaketi. Baada ya kitambo kidogo tarumbeta zikapigwa, nyimbo zikaimbwa, ndipo Mchungaji Sulemani akaja akitembea, akajitokeza. Na muda si muda mwajua, labda walianzisha m—mstari, labda walikuwa na namba, kadi, sijui jinsi walivyofanya hilo. Wa kwanza kuja, maskini Malkia anasema, “Sasa, nitaona sasa. Nitaangalia tu nione kama hii ni kweli ama si kweli, nione kama hiyo kweli ni upambanuzi.”

¹⁷⁷ Huyu hapa maskini mtu mmoja akaja, labda alikuwa ni mwanamume. Na muda si muda mwajua, aliona ya kwamba Sulemani alikuwa ni mwanadamu tu, kwa hiyo akasema, “Sasa, nitaona mahali huyo Mungu alipo. Ninaona kuna mtu, lakini ninataka kujua mahali huyo Mungu wa Kimbinguni alipo.” Kwa hiyo, akamwangelia mtu huyo, “Naam, anatembea kama mwanadamu, anazungumza kama mwanadamu, anaonekana kama mwanadamu, yeye ni mwanadamu, hivyo tu. Lakini sasa, hayo yaliyo ya Kimbinguni yanatoka wapi?”

¹⁷⁸ Kwa hiyo, wakati mtu huyu aliposimama pale, muda si muda mwajua, roho ya upambanuzi ikamjia Sulemani, naye akamwambia siri za moyo wake. Ninawazia moyo wa maskini huyo Malkia ulianza kudundadunda upesi. Wa pili, jambo lile lile; aliyefuata, jambo lile lile; aliyefuata, jambo lile lile.

¹⁷⁹ Akaenda nyumbani usiku huo labda, na kuombea hemani mwake. Kesho yake akarudi, akaketi tena, akasema, “Ninaamini nitapata kadi ya maombi,” kwa hiyo yeye, ama kitu fulani, chochote kile, “Nitapanda juu.” Kwa hiyo basi, walininii... Hatimaye, namba ya—yake ikaitwa.

¹⁸⁰ Sasa, tungeweza kukaa muda mrefu juu ya jambo hilo, lakini ili kuokoa wakati, tunakaribia kufunga. Kwa kuwa wakati wake ulifika, ndipo hatimaye alipokuja mbele ya Sulemani, Biblia ilisema ya kwamba hakuna kitu alichotaka kujua alichofichwa Sulemani. Mungu alikimwagiza tu Sulemani, na kumwambia kila siri aliyotaka kujua. Hilo si ni zuri sana? Mnajua alichosema? Alisimama. Sasa, yeye hakurudi, na kusema, “Ninaamini ni telepathia ya kiakili. Ni—ninaamini ni...” La, la. Alisimama, naye akasema, “Yote niliyosikia yalikuwa ni mazuri sana, bali ni makuu kuliko vile nilivyodhani yalikuwa. Ni makuu zaidi kwa sababu yalifanya kazi kwangu.” Amina.

¹⁸¹ Yesu alisema, “Atasimama katika siku za mwisho pamoja na kizazi hiki na kuwahukumu kuwa wamekosa, kwa maana alikuja kutoka pande za mwisho za dunia ili asikie hekima ya Sulemani.” Ilikuwa ni kitu gani? Aliona kitu halisi. Ulimwengu unaishi leo kwa ajili ya kitu halisi. Hivi hamwoni hivyo? Wanataka kitu kilicho na msingi.

¹⁸² Si muda mrefu uliopita, mimi... Nami nitafunga kwa hadithi hii ndogo ninayojiandaa kuwasimulia sasa. Nilikuwa nikiwinda kwenye misitu ya kaskazini. Jinsi ninavyopenda kuwinda! Nami niliwinda pamoja na jamaa aliyeitwa Call, mtu mzuri sana, bali alikuwa ndiye mtu katili sana niliyepata kuona inapofikia kuwa na moyo katili. Angewapiga risasi maskini watoto wa kulungu apate tu kunifanya nijisikie vibaya sana juu yake. Nami ningesema, “Usifanye hivyo, Buddy, usifanye hivyo.”

Anasema, “Aa, Mhubiri, jirudie, wewe ni mwoga sana. Hiyo ndiyo shida yenu ninyi wahubiri.”

¹⁸³ Nikasema, “La.” Nikasema, “Siamini ni kosa kumpiga risasi mtoto wa kulungu kama,” nilikuwa mlinzi wa wanyama pori kwa miaka mingi, nami nikasema, “kama sheria inasema unaweza kumpiga risasi mtoto wa kulungu, lakini usifanye hivyo kikatili. Ibrahimu alimwua ng’ombe, ndama na kumlisha Mungu. Ni sawa kumwua mtoto wa kulungu kama sheria inasema hivyo, lakini si kuua tu wanane ama kumi ili tu kumfanya mtu ajisikie ninii. . . , uh, vibaya.”

¹⁸⁴ Naye alikuwa na macho kama tu ya mjus, kwa vyovyote vile, yeye, na yeye—yeye daima... Sikulimaanisha hilo hivyo, yeye kwa namna fulani ni jamaa wa kipekee, na—naye alikuwa akitaka kunifanya nijisikie vibaya sana, kwa hiyo akaniambia... Siku moja alikuwa huko juu, nikaenda kuwinda pamoja naye, alikuwa na filimbi ndogo. Alikuwa ameifanya filimbi hii ndogo, angeweza kuipuliza ikasikika kama mtoto mchanga wa kulungu akimlilia mama yake (Mwajua, jinsi mtoto wa kulungu alivyo, maskini jamaa huyo mdogo.), naye humwita mama yake. Nikasema, “Bert, hungefanya jambo kama hilo, siuyo?”

Akasema, “Aa, Billy,” kasema, “jirudie. Hivyo ndivyo ilivyo kwenu ninyi wahubiri, ninyi ni waoga mno.”

Nikasema, “La, la, Bert. Hilo—hilo si sawa,” nikasema, “usifanye hivyo.”

¹⁸⁵ Vema, alikuwa mwindaji mzuri, haikukubidi kumtafuta, alijua mahali alipokuwa. Na kwa hiyo, tungetoka, nasi tulikuwa na wakati mzuri sana pamoja. Alikuwa mzuri, loo, ana shabaha sana. Na kwa hiyo, tu—tukawinda asubuhi moja. Daima tungeweka chokoleti moto kwenye jagi ya themosi *huku* nyuma, na kulikuwa na yapata inchi sita za theluji ardhini, hali ya hewa nzuri ya kufuatilia. Nasi tukapanda kupitia Njia ya mlima kisha tukapanda kwenye safu ya Urais. Ikafikia yapata saa tano mchana, nayo majira yalikuwa yameenda sana.

¹⁸⁶ Ndipo wakati hao kulungu mkia mweupe, mnanena kuhusu Houdini kuwa bingwa wa kutoroka, mnapaswa kuona mmoja wao. Kwa hiyo, wa—wao kweli wanaweza kutoroka. Na kwa hiyo, kichaka ni kinene, nao wanaweza kuingia chini ya kichaka, na kadhalika, na kujificha mchana kutwa, kisha wanakula

malishoni usiku. Kwa hiyo, basi hawatatoka, isipokuwa uwafukuze tu.

¹⁸⁷ Kwa hiyo, Bert akasimama kwenye ule uwazi mdogo, karibu, loo labda, mkubwa kama sakafu kuu ya ukumbi huu, akasimama yapata saa tano, kisha akaanza kuingiza mkono nyuma kotini mwake, nami nikawaza, “Vema, ni wakati tu wa kula sambusa, ndipo tutengane, naye aende njia moja, nami niende nyingine.” Tulikuwa tumetembea kwa yapata saa tatu ama nne, na moja kwa moja mlimami, ndipo angeshuka aende upande huo mwingine, nami ningepitia huo mwingine, nasi tungekutana wakati fulani usiku huo kwenye—kwenye kambi yetu ya kawaida, tuliyopiga.

¹⁸⁸ Kwa hiyo nikamwona akiingiza mkono nyuma, nami nikafikiri alikuwa akitafuta chokoleti yake moto, ndipo alipoutoa, alikuwa na filimbi hii. Nami nikasema, “Bert, hutakilipua kitu hicho.”

¹⁸⁹ Akasema, akaniangalia kwa hayo macho yanayofanana na ya mjusi, akasema. . . Naye akaiweka kinywani mwake namna *hii*, na kuipiga. Ilisikika tu kama mtoto wa kulungu anayemlilia mama yake. Nami kamwe. . . Sikudhani ingefanya kazi.

¹⁹⁰ Kwa hiyo yapata tu wakati huo, upande wa pili wa huo uwazi, jike mkubwa mno wa kulungu akasimama; alikuwa ni kitu cha kupendeza. Naye alikuwa karibu vya kutosha hata niliweza tu kuona macho yake makubwa, ya hudhurungi. Na—nami nikamwangalia, akaniangalia na kutabasamu, kitu kama hicho. Nikasema, “Bert, kweli hutamwua mama huyo, sivyo?” Naye akaniangalia namna *hiyo*, naye akainama na kuipiga tena.

¹⁹¹ Sasa, kwa kawaida, hilo si la kawaida kwa kulungu kufanya hivyo. Ndipo alipoipiga tena, mama huyo akaingia moja kwa moja kwenye uwazi huo. Sasa, hilo si la kawaida, hawatafanya hivyo, hata wakati wowote ni vigumu, hasa sana msimu wa kuwinda, bunduki zikiisha kufyatuliwa, na kadhalika. Lakini alitoka akaingia kwenye huo uwazi. Ilikuwa ni kitu gani? Yeye hakuwa mnafiki, alikuwa ni mama. Kulikuwa na kitu ndani yake kilichokuwa halisi, kilikuwa ni mama. Mtoto mchanga alikuwa katika shida, naye alitaka kujua mahali mtoto wake alipokuwa. Haikuleta tofauti yoyote ilikuwa ni hatari jinsi gani, hiyo hatari hata haikuisumbua akili yake.

¹⁹² Ninaweza kuona hayo masikio makubwa sasa, yamesimama tu namna *hiyo*, kinywa hicho kikitafuna namna *hiyo*, hayo macho makubwa ya hudhurungi yakiangalia kila mahali. Akaniangalia namna hiyo, na kuvuta juu, kamwe hatukubeba bunduki zetu zikiwa na risasi, na kwa hiyo akavuta, akavuta chini huo wenzu wa risasi ukubwa wa .30-06, 180, uyoga, akailenga namna *hiyo*, nami nikawazia, “Loo, jamani!” Nikawaza, “Bert, unawezaje kufanya hivyo?” Nikasema,

"Mama huyo wa thamani akimtafuta mtoto wake mchanga!" Nami...

¹⁹³ Kwa namna fulani a—akacheka tu, na kulenga, hodari wa shabaha. Nilijua, jamani, katika sekunde moja ama mbili angeulipulia mbali huo moyo wa thamani na mwaminifu kutoka kwake, maana alikuwa ni mtu hodari sana wa shabaha. Nikawaza, "Anawezaje kuwa mwovu hivi? Huku mama huyo akitoa onyesho hilo la upendo halisi wa mama!" Mtoto wake alikuwa katika shida, hakuajali hilo.

¹⁹⁴ Ndipo komeo liliposhuka, na bunduki ikainuliwa, kulungu akamwona mwindaji, akaangalia, naye akaruka. *Ruka* linamaanisha, "akaruka tu," mwajua, kwa dakika moja tu. Ndipo akamwanguka mwindaji, lakini alikuwa amemsikia mtoto huyo mchanga, naye alijua ya kwamba kifo chake kilikuwa moja kwa moja juu yake. Lakini je, alikimbia? La, bwana. Alikuwa akiangalia kuona mahali mtoto huyo mchanga alipokuwa, kwanza. "Loo," nikawazia, "uaminifu wa namna hiyo, mwaminifu hivyo! Na huo moyo wa thamani, mwaminifu, Bert, utaulipua utoke kwa mama huyo, namna hiyo?"

Yeye, nilimwona akilenga chini namna *hii*, nami nikawazia, "Si—siwezi kabisa kuiangalia."

¹⁹⁵ Nikageuza mgongo wangu, nami nikawazia, nikasema, "Baba wa Mbinguni, anawezaje kuwa mwovu hivyo, na hata hivyo awe mtu mzuri hivi kwa njia moja, kisha awe katili sana moyoni mwake kuulipulia mbali moyo wa thamani wa mama huyu, huo moyo mwaminifu ukidunda pale kwa ajili ya mtoto huyo mchanga? Vipi, kwa nini—kwa nini aweze kufanya jambo kama hilo?"

¹⁹⁶ Nami nikaona, bunduki haikufyatuka, ndipo nikangojea, nikangojea, nikawaza, "Kwa nini haikufyatuka?" Nikaangalia kote, nao mtutu wa hiyo bunduki ulikuwa ukienda *hivi*.

¹⁹⁷ Ndipo akageuka na kuniangalia, nayo macho hayo yalikuwa yamebadilika, machozi makubwa mno yalikuwa yakimtoka, yakitiririka mashavuni mwake. Akatupa hiyo bunduki chini, na kunishika kwenye mguu wa suruali, akasema, "Billy, yamenitoshia." Akasema, "Niongoze kwa huyo Yesu unayenena habari zake."

¹⁹⁸ Ilikuwa ni kitu gani? Aliona kitu halisi, aliona kitu ambacho hakikuwa cha kuigiza, aliona upendo halisi wa mama ambao utatembea moja kwa moja mbele ya mauti. Haikuwa ni mahubiri niliyohubiri, haikuwa ni wimbo ulioimbwa, ilikuwa ni onyesho la kitu kilichokuwa halisi sana, kwamba aliona kitu halisi. Basi uaminifu wa mama huyo ukamwongoza mtu huyo, yeye ni shemasi katika kanisa la Kibaptisti kule sasa. Upendo wa mama ukiwa halisi!

¹⁹⁹ Loo, rafiki mwenye dhambi, ama mfuasi vuguvugu wa kanisa, hivi hungetaka kuwa na upendo wa Yesu Kristo

kuuonyesha ulimwengu, mwaminifu kwa Kristo kama yule mama alivyokuwa kwa mtoto wake mchanga? Waweza kuinua mkono wako? Useme, “Niombee, Ndugu Branham, kwamba nitakuwa Mkristo wa namna hiyo.” Inueni mikono yenu, kila mahali. Mungu awabariki. Mungu awabariki. “Ninataka kitu halisi, Ndugu Branham, ninataka kitu kinachodumu. Ninataka kuwa Mkristo kadiri yule kulungu alivyokuwa mama.” Inueni mikono yenu juu sana sasa, ili niweze kuomba. Mungu awabariki. Mungu awabariki.

Na tuinamishe vichwa vyetu.

²⁰⁰ Baba wa Mbinguni, mikono ilikuwa mingi sana nisingeweza kuihesabu, ilikuwa kote kote, kila mahali, huko juu kwenye roshani, na mbele, na nyuma, na kandokando, na loo, kila mahali, kote kupitia kwenye sakafu kuu. Waliinua mikono yao, Bwana, kwa sababu kwamba wa—wanakuamini Wewe. Wanataka kitu halisi, wa—wanataka kitu ambacho si cha kuigiza, kitu ambacho ni—ambacho ni halisi kabisa. Ninaomba ya kwamba uwape Hiyo, Baba. Wape Roho Mtakatifu halisi. Jalia warudi kanisani mwao wakiwa na furaha na kushangilia.

²⁰¹ Sasa, imeandikwa katika Neno, Yohana Mtakatifu 5:24: “Yeye ayasikiaye Maneno Yangu,” hilo ndilo nimekuwa nikihubiria, “na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa milele, wala hataingia Hukumuni, bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani.” Sasa, Baba, ninashikilia hilo, hilo ni Neno Lako, ninaliweka mbele Zako, na Wewe uliye na nguvu zote, ujuaye yote, na unajua kila mkono ulioinuliwa.

²⁰² Kwa nini wakainua mikono yao juu? Kwa sababu kuna roho ndani yao, na kuna Roho aliyesimama karibu nao aliyesema, “Umekosea, unataka kuwa Mkristo wa namna hiyo. Inua mkono wako sasa, nami nitakuokoa.” Nao wakainua mkono wao. Walifanya uamuzi, uamuzi huo ulikuwa kwamba wanatamani kuishi maisha tofauti.

²⁰³ Nawe ulisema, “Yeye ayasikiaye maneno Yangu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa milele, wala hataingia Hukumuni, bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani.” Pia ulisema, “Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu, asipovutwa na Baba Yangu. Na wote alionipa Baba, watakuja Kwangu. Nitampa Uzima wa milele, na kumfufua katika siku ya mwisho.”

²⁰⁴ Sasa, Baba, hilo ni Neno Lako. Na kama mtumishi Wako usiku wa leo, ni—ninadai kila mmoja wao hao watu kwa ajili Yako, ninawadai, kila mmoja. Ninaomba, Mungu, kwamba kwa kuwa wamekuja Kwako sasa, kwenye Chemchemi hii iliyojaa Damu, kwamba wataokolewa salama, nao wataondoka hapa usiku wa leo, na kutafuta na kuupata ubatizo wa Roho Mtakatifu ambao utawatia muhuri mbali na mambo ya ulimwengu. Tujalie.

205 Huku tumeinamisha vichwa vyetu, hakuna mahali pa kuita wito wa madhabahuni hapa, lakini nashangaa tu kama kila mmoja wenu aliyeinua mkono wake ungesimama tu kwa miguu yako. Ninyi wengine endeeleni kuinamisha vichwa vyenu. Simameni tu kwa miguu yenu kwa dakika moja tu. Ninaamini mlikuwa waaminifu. Simameni, kila mmoja aliyeinua, kama waliinua mkono wao, wasimame, wote walioinua mikono yao, kila mahali. Hiyo ni kweli. Njoni huku, kila mahali. Endeeleni tu kusimama kwa muda kidogo kwa ajili ya maombi. Kila mtu aliyeinua mkono wake, asimame. Vema. Ni hayo tu sasa, kila mmoja? Vema.

206 Katika Uwepo wa Utukufu huu wa Shekina wa Roho Mtakatifu, ambapo sasa mmeamini kwa sababu ya kuhubiriwa kwa Neno, na kudhihirishwa kwa Roho Wake, siamini, ninaamini kila mmoja wenu kwa moyo wangu wote, siamini kwamba uliinua tu mkono wako kwa ajili tu ya raha ya kuuinua. Ninaamini kwamba uliunua kwa sababu ulikuwa mwaminifu, uliamini kwamba ulikuwa umekosea. Na kama uko tayari kukiri kwamba umekosea, na kusimama kama vile umefanya sasa, basi ninaamini ya kwamba Mungu na Neno Lake, ambaye hutimiza kila Neno aliloahidi, amekusamehe dhambi yako.

207 Si kwa sababu ati unajisikia hivyo, si kwa sababu unastahili, bali kwa sababu Yeye aliahidi jambo hilo, ni Neno Lake. Nawe uko tayari, na unajua ya kwamba wewe, umekuwa makosani, bali kweli unaamini ya kwamba Yeye alikufa, na hayo mawingu makubwa meusi yaliyotanda juu ya msalaba siku hiyo, Yeye alikuwa akiitetea hukumu yako, na bila kitu chochote, unakubali huo kama msamaha wako.

208 Kama utafanya hivyo, kukubali neema Yake kwa ajili ya msamaha wako, waweza tu kumwinulia mkono wako, kila mtu aliyesimama? Inua mkono wako, hayo tu ndiyo ninayokuomba ufanye, moyoni mwako tu. Mungu awabariki. Kuna asilimia mia moja, kila mmoja wenu.

209 Sasa, ninawatakeni ninyi watu ambao ni Wakristo mwinue kichwa chenu, na kugeuka tu na kupeana mikono na kila mmoja wao aliyesimama, na kusema, “Karibu katika Ufalme, ewe msafiri wa thamani.” Peaneni mikono nao, ninyi Wakristo. Waambieni ya kwamba u—unamshukuru Mungu. Kila mmoja wenu, aseme, “Naam, ninashukuru.” Waalike kanisani mwako sasa. Waambie, “Njoni kanisani mwangu. Njoni pamoja nasi, na, mpate kupokea ubatizo wa Kikristo, mpate kumpokea Roho Mtakatifu.” Hiyo ni kweli. Loo, Yeye si ni wa ajabu? Sasa, hebu na tumshukuru tu Bwana sasa.

210 Baba wa Mbinguni, tunakushukuru Wewe kwa ajili ya nafsi hizi. Huenda kamwe nisipeane mikono nao hapa duniani tena, kamwe nisiwe na nafasi labda, natumaini nitakuwa nayo, lakini nisipoipata, katika siku hiyo wakati ukungu umepungua, ile

Meli ya Kale ya Sayuni inavuma, tutakapoanza kupanda hiyo meli, nitakutana nao, nitawaona kule, Bwana, wakiwa na tiketi zao mkononi mwao, waseme, “Nilikuwa Long Beach, Ndugu Branham, Jumapili hiyo usiku.”

²¹¹ Ee Mungu, jinsi nitakavyokuwa na furaha kujua ya kwamba nitakutana nao kule! Vijana watakuwa wazee—vijana watakuwa . . . Wazee watakuwa vijana huko milele, wala hakutakuwa na magonjwa tena, na huzuni, wala mauti. Utakuwa ni wakati mzuri jinsi gani! Ninakushukuru kwa ajili ya jambo hili, Baba. Wao ni Wako, nami ninawakabidhi Kwako kama nyara za Yesu Kristo, Roho Wake na Uwepo Wake hapa usiku wa leo. Ninawakabidhi Kwako, Baba, katika Jina la Yesu Kristo, kwa sababu wao ni zawadi za upendo kwa Kristo. Amina.

²¹² Sasa, mnaweza kuketi, na Mungu awabariki. Sasa, kabla hatujabadilisha mahali pa mkutano kwa ajili ya mstari wa maombi, hebu na tuimbe tu mara moja, sivyo, sote pamoja? Kabla hatujaitisha mstari wa maombi, “Nampenda, nampenda, kwani alinipenda kwanza.” Vema, tunaweza kuimba?

Nampenda, nampenda
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Kwenye ninii ya Kalvari . . .

²¹³ Loo, hilo si linasikika zuri, ndugu? Laiti mngaliweza kuwa hapa juu na kuusikiliza huo. Si ni mzuri huo? Sasa ninawatakeni mwinamishe vichwa vyenu na kuuimba, kwa upole na utamu, kwa sauti yako nyembamba, ama besi, popote unapoitimia. Imbeni tu kwa mtindo wa kale, mtindo wa kishamba sasa.

Nampenda, . . .
Kwani Yeye . . .
Na kununua wokovu . . .
Juu ya . . .

²¹⁴ Loo, Yeye si ni mzuri? Loo, hivi hatumpendi tu? Ajabu! Sasa, marafiki, ninajua ni—niliwaweka kwa muda mrefu kidogo, lakini hii ni Jumapili usiku, tunaomba mtupe yapata dakika kumi na tano zaidi ama ishirini, tutaitisha mstari wa maombi.

²¹⁵ Sasa, ni wangapi wanaoamini ya kwamba Maandiko yanafundisha ya kwamba Yesu ni yeye yule jana, leo, na hata milele? Ni wangapi wanaojua ya kwamba Biblia inasema ya kwamba Yeye ni Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu? Hiyo ni kweli. Kama Yeye ni yule yule jana . . . Basi ni wangapi wanaoamini ya kwamba sisi ni . . . tuko kwenye mwisho wa wakati wa Mataifa? Ni wasomaji wangapi wa Biblia, huku mmeinua mikono yenu, watapunga mkono namna *hii*, na—na kuamini ya kwamba Yeye aliahidi ya kwamba angefanya mambo yale yale kwa kumalizia kwa Mataifa, aliyofanya kwa Wayahudi?

216 Mnaona, jambo ndilo hili: Kama Mungu kamwe akiitwa jukwaani kufanya uamuzi, jinsi anavyoufanya, Yeye ni wa Milele, haina budi kuwa vivyo hivyo kila wakati anapoitwa tena. Kwa hiyo wakati alipoitwa duniani kuja duniani, kujitangaza Mwenyewe kuwa Masihi, kumalizia wakati wa Wayahudi na Wasamaria, Yeye hana budi kufanya jambo lile lile atakapokuja baadaye, Wayahudi walikuwa na miaka elfu nne, tumekuwa na miaka elfu mbili, mwishoni mwa wakati ajitokeze jukwaani na kufanya jambo lile lile. Hiyo ni kweli?

217 Vema sasa, ikiwa Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele, hana budi kuwa yeye yule kimsingi, yeye yule katika nguvu, yeye yule katika madhihirisho, kitu pekee ni mwili wa kawaida, mwili Wake uko kwenye mkono wa kuume wa Mungu Baba Mbinguni, ameketi kwenye Kiti cha Enzi. Unaamini hilo? Kuhani Mkuu, na sasa Roho Wake Mtakatifu yuko hapa, Roho ambaye alikuwa juu ya Kristo, ambaye ni Mungu, katika mwili wa mwanadamu, mwili wako, mwili wangu, kama vile Damu inavyotusafisha. Anahubiri Injili kupitia kwa mhubiri, anatabiri kupitia kwa nabii, na kufunua siri, mioyo, ananena kwa lugha, anafasiri lugha, na kila kitu kiko katika utaratibu. Unaamini hilo? Vema.

218 Vema, sasa hebu tuitishe mstari wa maombi. Sasa, aliniambia aligawa kadi za maombi, lakini nasema sijui ni zipi na ni wapi. Loo, Billy, wewe ni mdogo sana, sikuzote sikuoni. Vema, moja hadi mia moja, J. Vema. Namba moja. Hebu tuanze. Ni nani aliye na J, kama katika Jesus? J angalieni kwenye, ina J na namba fulani. J, namba moja, ni nani aliye nayo? Inua mkono wako. Una hakika? Vema. Njoo papa hapa, mama. Namba mbili, ni nani aliye na J, namba mbili? Je, waweza kuinua ninii yako . . . ? [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

219 . . . maisha yangu. Naye hatufahamiani, maana tuliinua tu mikono yetu, kwamba hatufahamiani. Sasa, simjui, wala yeye hanijui. Lakini sasa, yeye yuko hapa kwa kusudi fulani. Ni kitu gani? Yeye ni mgonjwa? Labda hivyo. Labda yuko hapa kwa ajili ya mtu mwingine, labda ni matatizo ya kinyumbani, labda ni—ni matatizo ya kifedha, labda ni kitu kingine, sijui. Mnaona? Si—sijui, Mungu anajua.

220 Sasa, kama amekuwa hapa ndani, kama kawaida, katika ibada za uponyaji, ningemwekea mkono wangu, niseme, “Mungu, mponye mwanamke huyu, mimi ni mwaminio, ninaomba itimizwe. Amina.” Sasa, mwanamke huyo ana haki ya kuondoka na kuamini. Kama aliamini hilo, hilo ni Neno la Mungu, kuweka mikono juu ya wagonjwa. Hiyo ni kweli? Angekuwa na haki ya kuamini hilo.

221 Lakini sasa vipi kama Roho Mtakatifu akija na kumfunulia jambo fulani lililoko ndani ya maisha yake, anamwambia yaliyompata? Na kama Yeye anaweza kumwambia, kwa usahihi, yale yamekuwa, hakika, angeweza kuamini mambo ya usoni

basi. Hiyo ni kweli? Sasa, ni wangapi wanaojua ya kwamba hivyo ndivyo Yesu alivyofanya? Inua mkono wako. Hivyo ndivyo alivyoahidi. Hiyo ni kweli kabisa.

²²² Sasa, kama Yeye yuko hapa. . . Sasa Yeye yuko hapa katika umbo la Roho Mtakatifu. Sasa, hii ni mandhari, kama vile tu kile kisima kilivyokuwa katika Yohana Mtakatifu 4, picha nzuri tena, mwanamume na mwanamke, mara ya kwanza kukutana maishani, mimi na mama huyu, kwa mara ya kwanza maishani kukutana, na sasa ni papa hapa ambapo hatujawahi kukutana hapo awali. Sasa, kama Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele, sasa, kitu fulani ingembidi kifunue kile kilichomleta hapa, naye angejua hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli, mama? *Mtu fulani* ingembidi kulifunua, itabidi *Kitu fulani* kuja na kufanya hivyo. Hiyo si ni kweli?

²²³ Vema basi, kama Yeye akija, sasa, huyu angeweza kusema, “Ni ibilisi.” Basi hiyo ni juu yake. Mnaona? Kama angesema ilikuwa ni Kristo, kuna ninii tu, ingebidi iwe ni nguvu za kiroho. Kama akisema ibilisi, basi angepata thawabu ya ibilisi; akisema Kristo, anapata thawabu ya Kristo. Lakini kama angesema ibilisi, na ilikuwa ni Kristo, basi amefanya nini? Amejitia muhuri, milele, kutoka kwenye Ufalme wa Mungu. Je, hivyo ndivyo Yesu alivyosema? “Roho Mtakatifu ajapo, kunena neno moja dhidi Yake, hutasamehewa kamwe,” haidhuru wewe ni nani.

Unasema, “Lakini ninahubiri Injili, Ndugu Branham.”

²²⁴ Vivyo hivyo na hao makuhani, walilelewa kupitia vizazi vya makuhani, na walikuwa wamehubiri Injili, ndipo Yesu akawaambia waziwazi, nao wakapoteza maisha yao. Hiyo ni kweli. Njia moja tu ya kumwendea Mungu, hivyo tu, hiyo ndiyo Njia ya Kweli na Nuru.

Sasa, kama ungeweza kusimama papa *hapa* nje. Haikubidi kusimama. . .simama tu moja kwa moja upande huu, kusudi watu waweze kukuona na kuniona mimi.

²²⁵ Sasa, kwa kuwa. . .Sasa, hapa ni kama yule mwanamke kisimani. Sasa, mimi. . . Yeye siye yule mwanamke, wala mimi si Bwana Yesu, bali Roho Wake yupo hapa, na Yeye angejua, anaweza kumwambia. . .Sasa, kama Yeye angeninii. . .

²²⁶ Sasa, kama tungenesema, “Ndugu Branham, Yesu alifanya nini pale?” Vema, Biblia ilisema alikuwa na haja kupitia Samaria, sijui ni kwa nini. Baba alimtuma huko juu, kwa sababu Yeye alisema katika Yohana Mtakatifu 5—Yohana Mtakatifu 5:19, “Amin, nawaambia, Mwana hawezi kutenda neno Mwenyewe, ila lile amwonalo Baba analitenda.” Ni wangapi wanaojua Maandiko hayo? Yesu hakufanya jambo moja, mpaka Mungu alipomwonyesha katika ono jambo la kufanya. Hiyo ni kweli? Yohana Mtakatifu 5:19: “Amin, amin,” *kabisa, kabisa*, “nawaambia, Mwana hawezi kutenda neno Mwenyewe,

ila lile amwonalo Baba analitenda, ndilo atendalo Mwana vile vile.”

227 Sasa, basi kama mwanamke huyu aliyeinua mkono wake, kwamba hanifahamu, nami simfahamu, basi kama Roho Mtakatifu, kwa ahadi Yake, ni yale nimewafundisha, atakuja hapa na atafanya jambo lile lile alilofanya wakati huo, kufunua siri ya moyo wa mwanamke huyo, ama afanye vile alivyo, na kumwambia kile, kitu fulani kumhusu yeye mwenyewe, na kumwacha awe hakimu kama ni kweli ama si kweli, ni wangapi hapa ndani watamwamini Bwana Yesu Kristo kwa ajili ya uponyaji wenu? Na sasa, kote kila mahali inueni mikono yenu kama mtaamini. Kuna angalau alilimia tisini na tano.

228 Bila shaka wengine wasingeamini hilo, mnaona, haidhuru Yeye amefanya nini. Si kwa ajili ya wasioamini, ni kwa ajili ya waaminio tu. Kulikuwa na wengine waliosimama katika umati Wake ambao hawakuamini. Hilo halitamdhuru mwaminio, la, tayari wanajua ni kweli.

229 Sina fununu hata—hata—hata kidogo ni kwa nini uko hapa, bali Mungu anajua kilichokuleta hapa. Kama atanifunulia, basi utajua kama ni kweli ama si kweli, lolote afanyalo.

230 Sasa, naam, kama wasikilizaji wangali wanaweza kuisikia sauti yangu, ile Nuru mnayoiona kwenye picha imesimama kati yangu na huyo mwanamke. Inaondoka kwangu. Kwa namna fulani ni Nuru inayokutuka, inayometameta.

231 Naam, naona, yeye, uchunguzi wake unaonyesha ya kwamba ana tumbo linalovimba, tumbo, ana tumbo mbaya, linavimba. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako.

232 Unaamini? Sasa, ulisema ungeamini kama Yeye angefunua hilo. Unaamini sasa? Basi ninii yake...ni...Na sasa sijui nilichomwambia, maana si mimi niliyemwambia. Ni kujitolea tu kwa Roho.

233 Sasa, ninaendelea kuhisi hilo katika kila mkutano, mtu fulani anasema, “Alibahatisha hilo, alibahatisha hilo.”

234 Hubahatishi mambo haya. Vema, angalieni kama ilikuwa ni kubahatisha:

235 Anaonekana kuwa mtu mzuri. Wewe ni Mkristo, ninaweza kuihisi Roho yako, naona kwamba umekaribishwa. Jambo lile lile ambalo Yesu alimwambia Nathanaeli, Mwisraeli. Sasa, hebu tuone kama chochote kile, naam, ninaiona ikiwa tena, ilikuwa ni ugonjwa wa tumbo, tumbo linalovimba, Yeye alisema. Hiyo ni kweli, hivyo ndivyo daktari alivyosema, tumbo linalovimba. Halafu basi hapo, hili hapa jambo lingine, kwamba una namna fulani ya ugonjwa wa rektamu. Hiyo ni kweli. U—unafikiri ni kitu kama mzio, ama namna fulani ya hisia za mwasho. Hiyo ni kweli, basi. Hakuna tiba yake, hiyo ni kweli, bali iko katika Kristo. Kama Mungu ataniambia kile...Ninaona jina

lako kwenye karatasi ile pale, Yeye amenitangulia, ninamwona amesimama pale, utaniamini mimi kuwa ni nabii Wake? Bibi Martin, unaweza kuendelea. Imekwisha sasa, unaweza kwenda nyumbani, upate afya, unaona.

236 Sasa, ewe mkosoaji, vipi kuhusu hilo?

237 Sasa, wewe mwaminio huko nje, amini kwa moyo wako wote sasa. Amini tu, usiwe na shaka, amini kwa moyo wako wote. Sasa, iweni watulivu, kaeni tu mahali penu, kaeni kimya.

238 Sijawahi kumwona mwanamke huyo, mnaona. Kamwe sikumponya, Mungu alimponya. Yeye alimponyaje? Imani yake mwenyewe ilifanya hivyo. Uponyaji ulikuwa tayari umekamilika pale Kalvari, wokovu wako ulikamilika pale Kalvari. Unajuaje jambo hilo? Hiyo ni kweli? Yote unayopaswa kufanya ni kuukubali.

239 Sasa, huyu hapa mama mwingine. Nasi tulikuwa...mara yetu ya kwanza, hatufahamiani. Mungu anatujua sote wawili hata hivyo, sivyo? Vema basi, kama Bwana Yesu atanifunulia jambo ambalo—ambalo mimi...

240 Bila shaka mnaniona nikininii, nikionekana namna hiyo. Hiyo ni kwa sababu tu limeninii, limenifanya dhaifu, ono. Mnaona, hili kusanyiko linajua, mtu yeyote anajua, Yesu, mwanamke aligusa vazi Lake, Yeye akasema amekuwa, nguvu zilitoka. *Nguvu* ni “uweza,” mnajua hilo. Naye Danieli aliona ono moja, akafadhaika kichwani mwake siku nyingi. Vema basi, kama Yesu akiwa ni Mwana wa Mungu, kama mwanamke mmoja alingusa, vema, ingefanya nini kwangu, mnaona, mimi, mwenye dhambi aliyeokolewa kwa neema? Kwa sababu Yeye alisema, “Mambo nifanyayo Mimi ninyi nanyi mtayafanya, mengi kuliko haya mtayafanya.” King James inasema *makubwa zaidi*, lakini ukichukua tafsiri ya kawaida, inasema *mengi zaidi*. Unaona? “Mengi zaidi mngeweza kufanya,” ni ahadi Yake.

241 Sasa, kama Roho Mtakatifu atanifunulia shida yako, ama kitu fulani, kama alivyowafanyia wale wengine waliopita, je, utaamini kwa moyo wako wote?

Je, ingesababisha kusanyiko kuamini kwa moyo wao wote?

242 Mnaona, Mungu hafanyi hivi kwa ajili ya kujionyesha, Yeye hufanya hivi kwa sababu aliahidi angelifanya, na kwa ajili ya utukufu Wake. Mnaona? Nami ninawaambia, si mimi, sijui hata jambo moja, ninaushika mkono wangu hapa mbele za Mungu na Biblia hii hapa, mwanamke huyu ni mgeni kwangu. Ninyi nyote ni wageni, nijuavyo mimi. Lakini kama Mungu atanifunulia kwa Roho Mtakatifu...

243 Sasa, Biblia ilisema, “Neno la Mungu ni kali kuliko upanga ukatao kuwili, Mtambuzi wa mawazo ya moyo.” Sasa, Yesu, wakati alipokuwa hapa duniani, Yeye alikuwa ni Neno, sivyo? Hiyo ndiyo sababu angeweza kutambua mawazo, kutambua, na

kadhalika, Yeye alikuwa—Yeye alikuwa ni Mungu-Nabii. Hiyo ndiyo sababu manabii, wangeweza kutambua? Kwa sababu walikuwa ni Neno la Mungu. “Neno la Mungu lilimjia nabii.” Hiyo ni kweli, wasikilizaji? Mnaona?

²⁴⁴ Sasa, kama Neno la Mungu lingali linakuja, basi Neno la Mungu linaweza, Waebrania inasema, “Neno la Mungu ni Mtambuzi wa mawazo,” Neno Lake, ahadi Yake inapoingia katika mwili wa mwanadamu hulifanya Mtambuzi wa mawazo ya moyo.

²⁴⁵ Sasa, huko hapa kwa ajili yako mwenyewe, uko hapa kwa ajili ya mtu mwingine, mume wako. Hiyo ni kweli, sivyo? Yuko katika hali ya kufa. Unaamini Mungu anaweza kuniambia ana tatizo gani? Kansa ya kibofu. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Utaamini ya kwamba Mungu atamponya? Nitaombea jambo lile lile. Hebu niweke mikono yangu juu yako, nawe umwakilishe.

²⁴⁶ Bwana Yesu, mwokoe mtu huyu, litimize, Baba, ninaomba, kwa unyenyekevu, kama mtumishi Wako, katika Jina la Yesu. Amina.

²⁴⁷ Mungu akubariki, Dada. Sasa, usiwe na shaka. Unaamini hilo sasa? Yesu alisema, “Kama ulivyoamini, ndivyo itakavyokuwa kwako.” Amini.

²⁴⁸ Hakuna mtu atakayejua kamwe hilo linakufanyia nini. Mnaona? Sasa kusanyiko linaonekana limepofushwa kwangu. Unaona? Sasa, iweni tu na imani sasa, na hebu. . .

²⁴⁹ Je, wewe ndiye mtu anayefuata? Mimi na wewe hatufahamiani, nadhani, sisi kwa sisi. [Dada huyo anasema, “Nilikuwa kwenye mstari wa uponyaji hapo awali.”—Mh.] Loo, umekuwa kwenye mstari wa uponyaji—katika mstari wa uponyaji hapo awali, mahali pengine. Katika mji mwingine, ama. . .? Katika Mtaa wa Ziwani, huko California, katika. . . Loo—loo, nilikuombea hapo awali kwenye Mtaa wa Ziwani. Imekuwa muda gani? Loo, ni miaka mingi iliyopita. Kwa hiyo tusingefahamiana? La. Lakini Mungu anatumia sote wawili. Nawe unaamini ya kwamba Mungu angeweza kunijulisha *kitu kingine*. . .? Je, Yeye alikuja. . .? Bila shaka alikuja vivyo hivyo, jinsi ilivyokuwa. Basi uko hapa kwa ajili ya jambo lingine sasa. Sasa, ungekuwa na imani basi, sivyo? Una imani, vema, kama Bwana atalifunua. Vema. Ninatumia ya kwamba atafanya hivyo.

²⁵⁰ Huko hapa kwa ajili yako mwenyewe wakati huu, uko hapa kwa ajili ya mtu mwingine, ndugu, mgonjwa sana, sana, karibu na kufa. Nami nitakwambia jambo fulani unalojua, ili upate kuniadini mimi kuwa ni nabii Wake, ama, mtumishi Wake, samahani. Hilo neno *nabii* huwaduwa watu, unaona, hiyo ndiyo sababu mimi. . . Lakini, ni mke wake, yuko katika hali mbaya. Yuko karibu kupatwa na fadhaa, kwa sababu ya

kumtunza. Una hisia ya ajabu sana juu yako sasa, sivyo? Chukua lesio hiyo uliyo nayo mkononi mwako, huku hisia hiyo ikiwa juu yako na kuiweka juu yake. Watapona. Usiwe na shaka. Amina. Mungu akubariki.

Unaamini kwa moyo wako wote, bado? Usiwe na shaka, mwamini Mungu.

²⁵¹ Uliyeketi papo hapo, shinikizo la chini la damu, mama anayeniangalia. Una kadi ya maombi? Huna. Vema, ni sawa, Yeye tayari amekuita, ninauona sasa. Inakubidi uongezewe damu. Hiyo ni kweli. Lakini nilipokuwa nikizungumza na mwanamke huyo, jambo fulani lilikupata, hisia ya ajabu sana ilikupitia. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako, maskini mama huyu aliyeketi papa hapa mbele. Vema. Nawe ulisema moyoni mwako, “Bwana, na iwe ni mimi, usiku wa leo.” Sasa, simama kama mambo hayo ni kweli, simama kwa miguu yako. Shida zako zimekwisha sasa, Yesu Kristo anakuponya.

²⁵² Ninataka kuuliza kusanyiko jambo moja: Mwanamke huyo aligusa nini? Simjui, sijawahi kumwona maishani mwangu. Kama hatufahamiani, pungu mkono wako, kwa mmoja... namna *hii*, Dada, pungu mkono wako namna *hii*, kusudi watu wajue ya kwamba hatufahamiani, sikujui.

²⁵³ Aligusa nini? Kuhani Mkuu. Yuko yadi ishirini kutoka kwangu. Hakunigusa kamwe, sivyo? Lakini aligusa *Kitu fulani* kilichonena kupitia kwangu, na kumwambia kile alichokuwa akiombea, yale aliyosema, na jinsi alivyojisikia. Hiyo ni kweli? Unaamini sasa, kwa moyo wako wote?

²⁵⁴ Sasa, msisogee, tafadhali msisogee. Mnaona, mkifanya hivyo, mnaona... Mnaona watu hawa waliosimama *hapa*? Wanaangalia kila hatua ninayochukua, na mara watakapoona kwamba nina ya kutosha, wataniondosha jukwaani. Kwa hiyo, ku—kusogea, husumbua. Unaona, ninawasiliana na roho yako, hivyo ndivyo ni—ninavyojaribu kufanya. Nipo hapa nikijaribu kuwasaidia. Kama wewe ni... Hakuna kitu kitakachoharibika, mtawahi basi lenu, tulieni tu. Ngoja tu, wawili au watatu tu zaidi, ama chochote kile, hebu...

U hali gani? Hatufahamiani. Sikujui, lakini Mungu anakujua. Kama...

²⁵⁵ Ni wangapi hawa ambao wamepitia? Wametosha kwa ajili ya thibitisho? [Ndugu mmoja anasema, “Wawili.”—Mh.] Ati wawili? Ninii tu, nilifikiri nilikuwa... dazani moja wamepitia, sasa. Vema, nilihisi ni wengi, labda ni mimi tu. Vema.

²⁵⁶ Wewe, Dada, Mungu anaujua moyo wako, Yeye anaujua moyo wangu. Lakini kama Yeye, bila shaka yoyote, sisi tukiwa hatufahamiani, ajifunue Mwenyewe kwetu, itakufanya uamini?

Itawafanya wasikilizaji waamini? Vema. Ni wangapi wanaojua ya kwamba mimi... haiwezekani kabisa kwangu kufanya hivyo? Hebu tuone mikono yenu. Unaona?

²⁵⁷ Sasa, huku mikono yenu ikiwa chini, ni wangapi wanaokubali Hilo kuwa ni Yesu Kristo kulingana na ahadi Yake na Neno Lake? Inueni mikono yenu. Unaona? Hiyo ni kweli, ndugu yangu, dada. Ninawaambia kweli, mnaona, hili ni Neno Lake. Labda ni ajabu kidogo kutokana na yale ambayo mumewahi kuona, bali ni ahadi Yake, Yeye aliahidi angefanya hivyo.

²⁵⁸ Sijui uko hapa kwa sababu gani. Sijawahi kukuona, kwa hiyo basi ingekuwa... Si—sina fununu ya kile kilichokuleta hapa, lakini Mungu anajua kilichokuleta hapa. Anakujua, Yeye ananijua mimi, Yeye—Yeye anatumia sisi sote. Hiyo ni kweli? Lakini kama atanifunulia jambo fulani kukuhusu ambalo silijui, basi utajua linatoka Kwake. Umekuwa na kitu kama kiharusi, kinakusumbua. Hiyo ni kweli. Wewe ni Mswidi, sivyo? Tack så mycket. Ningeweza kuona hayo maji yakifingirika, nami ningeweza kuona mahali ulipotoka. Naam. Umekuwa na ajali nayo ikakufanya uzimie, nawe ulizimia kwa muda mrefu, siku kadhaa. Na halafu wewe, ungali una athari mbaya kutokana nayo. Hutakuwa nazo tena, hiyo iligeuka nuru moja kwa moja karibu nawe, Yesu amekuponya sasa. Nenda zako, ukapate afya.

Je, unaamini kwa moyo wako wote?

²⁵⁹ Sasa, mnasema, “Unawaangalia watu hao moja kwa moja, Ndugu Branham, unasoma mawazo yao.”

²⁶⁰ Sivyo. Hapa, njoo hapa, mama, gusa mkono wangu. Kama Mungu atanifunulia nikiangalia *huku* shida yako ni nini, utaikubali, sivyo? Ndipo ugonjwa wako wa moyo umekuacha, nenda zako tu ukishangilia.

²⁶¹ Unaamini hilo kwa moyo wako wote? Hapa, Biblia ilisema yule Malaika kule chini ambaye alikuwa ni Mtu aliyetiwa mafuta aliitwa Elohimu, kwamba alikuwa ameelekeza mgongo Wake kwenye hema. Hiyo ni kweli? Vipi kama nikigeuza mgongo wangu, nawe uombe? Ninaona ninii... 

61-0219 Malkia Wa Sheba
Long Beach Municipal Auditorium
Long Beach, California Marekani

SWAHILI

©2025 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org